Nipashe

Jumatano Julai 8, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580278

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

• Jifunze kuhusu Ualbino

• Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

215779502

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN




## Waziri pekee serikali ya kwanza Balozi Job Lusinde afariki dunia

UKURASA 3

# Makada 124 wa CCM vikumbo majimbo 9

UKURASA 2



Umati ukiwa kwenye kilele cha Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **Picha zaidi Uk. 8.** **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Membe atangaza kuwania urais

**ATAMBA** kuibuka kidedea, chama chake bado kitendawili, ACT- Wazalendo wamkaribisha *Endelea ukurasa 2*



## MAJINGE ACHUKUA FOMU YA URAIS CHADEMA

UKURASA 3

BAA LA CORONA



## 'Usichukulie poa unategemewa'

* **Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka**
* **Kaa kwa kuachiana nafari hatua 2 au 3**
* **Vaa barakoa**
* **Ukikohoa au kupiga chafya ziba mdomo**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu



MICHEZO SIMBA YAAHIDI FURAHA LINDI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Makada 124 watia nia majimbo tisa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

VITA vya ubunge mkoani Kilimanjaro vimepamba moto ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya makada 124 kuonyesha nia ya kuomba uteuzi wa kugombea nafasi hiyo katika majimbo tisa ya mkoa huo.

Mchakato huo unatokana na wabunge wote nchini, kumaliza muda wao wa uongozi kwa kipindi cha miaka mitano, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Jana, Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum, alisema hadi kufikia Jumatatu, ofisi yake ilikuwa imepokea jumla ya wanachama 124 wanaoomba nafasi hiyo.

"Tangu ilipotoka kauli rasmi ya kiongozi wetu ambaye ni Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, ambaye ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi ngazi ya taifa, na sisi kama wasaidizi wake naomba nitoe taaarifa kuhusu nmchakato unaoendelea hapa Kilimanjaro.

"Hadi kufikia Julai 6, mwaka huu, tumepokea jumla ya wanachama 124. Hawa ni wale wanaoonyesha nia yao ya kuomba uteuzi wa kugombea ubunge katika majimbo tisa ya mkoa wa Kilimanjaro."

Alitaja majimbo na idadi ya watiania kwenye mabano kuwa ni Moshi Mjini (8), Moshi Vijijini (22), Jimbo la Vunjo (13) na Jimbo la Same Magharibi (13).

Majimbo mengine ni Same Mashariki (16), Jimbo la Hai (8), Jimbo la Siha (7), Mwanga (23) 23 na Rombo (14).

Kutokana na idadi ya watia nia kuongezeka kila uchao mkoani humo, Mabihya alisema: "Kwa mujibu wa katiba yetu na kanuni za CCM, wakurugenzi wa uchaguzi ni makatibu wa chama wa ngazi husika.

"Kwa maana ya makatibu wa mikoa, makatibu wa wilaya, makatibu kata na makatibu wa matawi, hao ndio wakurugenzi unapofika wakati wa uchaguzi. Kwa hiyo tunaposema kupitapita maana yake watu waende ofisi za chama, huenda mtu alikuwa na dhamira ya kugombea, lakini alikuwa hajui wapi pa kwenda kusema dhamira hiyo," alisema

"Hivyo ni wakati muafaka wa kwenda kwenye ofisi za chama ili tuweze kuwatambua."

Juni 12 mwaka huu, CCM ilipuliza kipenga cha uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kwa kufungua dirisha la kuchukua na kurudisha fomu kwa wanaowania nafasi za udiwani, uwakilishi, ubunge na urais kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa wanaowania nafasi ya udiwani, uwakilishi na ubunge kwa Tanzania Bara na Visiwani, dirisha la kuchukua na kurudisha fomu, litafunguliwa Julai 14 hadi 17, mwaka huu.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akiwaonyesha waandishi wa habari, mkoani humo jana, silaha mbili aina ya bastola walizokamatwa nazo, Jumbe Kamugisha na George Semtego wote wakazi wa Dar es Salaam, walizodaiwa kuzitumia kuwatishia watu wakati wa kuwapora magari maeneo mbalimbali hapa nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mkutano CCM wavuta wageni 3,000 Dodoma

**Na Waandishi Wetu, DODOMA**

MAANDALIZI ya vikao vikubwa vya Chama Cha Mapinduzi (CCM), yamepamba moto jijini Dodoma, yakichagizwa na upambaji wa bendera za chama hicho kwenye maeneo mbalimbali ya jiji hilo jipya.

Jeshi la Polisi limeonya watu watakaojitokeza kufanya uhalifu wowote wakati wa vikao hivyo vinavyotarajia kupeleka wageni takribani 3,000 jijini.

Vikao hivyo vinavyotarajiwa kuanza mwishoni mwa wiki hii, vinalenga kumthibitisha mgombea wa urais wa Tanzania kwa tiketi ya chama hicho, Dk. John Magufuli na kuteua mgombea urais wa chama hicho kwa upande wa Zanzibar.

Nipashe jana ilishuhudia uwekaji wa bendera za chama hicho katika barabara mbalimbali huku nyumba za kulala wageni katikati ya Jiji la Dodoma zikiwa zimejaa kuanzia Julai 9 hadi 12 mwaka huu na wageni wengine kulazimika kutafuta malazi nje ya mji.

Akizungumzia maandalizi ya vikao hivyo, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, alisema jana kuwa yanakwenda vizuri na wajumbe watafika kuanzia Julai 9, mwaka huu.

"Mkutano utakuwa na wajumbe zaidi ya 1,800 na wageni zaidi ya 1,000. Mkutano mkuu wetu utaketi Julai 11 hadi 12 mwaka huu na maandalizi yote yamefanyika," alisema.

Alisema mkutano huo utatanguliwa na kikao cha Kamati Kuu (CC) na baadaye NEC na kwamba mkutano mkuu wa uchaguzi wa wagombea urais utafanyika katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete.

Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Gilles Muroto, jana alionya makundi ya kihalifu ambayo yatajitokeza katika kipindi hicho cha mkutano huo na kudai kuwa jeshi hilo limejipanga kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwapo wakati wote.

Alisema pia watashirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kuhakikisha suala la rushwa halipati nafasi.

"Tumeweka mtego ambao hawakutarajia, uzoefu unaonyesha kwamba mkutano huu umekuwa ukihudhuriwa na makundi ya wapambe wa wagombea, familia za wagombea, wapiga debe, wajasiriamali mbalimbali sambamba na watu wabaya ambao hutumia fursa hiyo kutekeleza azma yao ya vitendo vya uhalifu," alisema Muroto.

# Membe kuwania urais, ACT wamkaribisha

**Na Romana Mallya**

ALIYEKUWA Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, amesema atawania kiti cha urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kupitia chama cha upinzani ambacho hajakitaja.

Muda mfupi baada ya kurejesha kadi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) juzi, Membe alizungumza na baadhi ya wafuasi wake akisema: "Tutajiunga na chama na tutagombea uongozi wa juu wa nchi mwaka huu na mwezi wa kumi (Oktoba) na tutashinda.

"Sijakisema chama kwa sababu mabaraza ya hivyo vyama yanakutana. Siyo vizuri tukatangulia kujipa wakati mabaraza yale yanakaa kuanzia sasa kujadili suala la Rondo (kijiji anachoishi) na jibu litakuwa ndiyo.

"Ninawaomba tuvumilie saa na siku maana sisi tunafuata taratibu. Tayari tumewasharoga huko, tumeshapeleka vitu vyetu huko, sasa hivi wanakaa kwa starehe kabisa na wamenipigia simu wanasema wanapokea maombi yale," alisema. Wakati Membe akiyasema hayo, viongozi wa ACT-Wazalendo mikoa ya Lindi, Mtwara, Mkoa wa Kichama Selou na Pwani, jana walitoa tamko la kumwomba ajiunge na chama hicho.

Viongozi hao ni: Mwenyekiti wa ACT Mkoa wa Lindi na mjumbe wa Kamati Kuu, Isihaka Mchinjita; Mwenyekiti wa ACT Mkoa wa Mtwara, Alphonce Hitu; Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Kichama Selous, na Abdallah Mtalika; na Mwenyekiti wa ACT Mkoa wa Pwani, Mrisho Swagara.

Kwa mujibu wa tamko hilo, viongozi hao walikwenda Kijiji cha Rondo kuwasilisha ombi maalum kwa Membe kujiunga na chama chao.

Walikumbusha kwamba Juni 30, mwaka huu,wakati Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akihutubia wanachama katika mkutano wa ndani uliofanyika Kilwa Kivinje mkoani Lindi, alimwalika Membe kujiunga na vyama vya upinzani, ili kuongeza mshikamano kuhami demokrasia na kuleta mabadiliko ya utawala nchini.

"Kwetu wito huu ulikuwa ni hatua muhimu kuelekea mageuzi makubwa ya kisiasa nchini. Uamuzi wa Membe wa kurudisha kadi ya CCM tumeupokea kwa matarajio makubwa.

"Hii ni kwa sababu uamuzi huu unafungua milango kwa yeye kuchagua kujiunga na vyama vya siasa vya upinzani nchini ikiwa ataona inafaa," ilielezwa katika tamko lao hilo. Viongozi hao walisema wamekuwa wakifuatilia kwa umakini misimamo, mwelekeo na mitazamo ya Membe kuhusu demokrasia, haki na utawala wa sheria.

"Kwa hakika, tunaamini kuwa hayo ndiyo yaliyokufanya ufukuzwe CCM. Hata hivyo, mambo haya uliyoyapigania ukiwa ndani ya CCM ni hitaji kubwa la taifa letu, ndiyo maana sisi viongozi tumekuja hapa kukuomba ujiunge na chama chetu cha ACT-Wazalendo.

"Chama chetu kimejipambanua kwa kupigania haki, demokrasia, utawala wa sheria, ushirikiano wa vyama vya siasa na wadau wengine, ili kuleta mabadiliko ya kiutawala na kuhami demokrasia," walieleza katika tamko lao hilo.

HABARI KITAIFA

# Balozi Lusinde afariki dunia

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI pekee aliyekuwa amebaki katika Baraza la kwanza la Mawaziri wa Tanganyika chini ya Mwalimu Julius Nyerere, Balozi Job Lusinde (90), amefariki dunia.

Balozi Lusinde alifariki dunia katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, jijini Dar es Salaam alikopelekwa kwa ajili ya matibabu.

Aidha, taratibu za mazishi zinafanyika nyumbani kwake Dodoma na mwili wake unatarajiwa kuwasili leo kutoka Dar es Salaam.

Akithibitisha taarifa za kifo hicho, msemaji wa familia ambaye ni Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, alisema Balozi Lusinde amefariki dunia kutokana na kusumbuliwa na maradhi tangu Februari, mwaka huu.

"Kaka yangu amefariki (dunia) leo (jana) alfajiri katika Hospitali ya Muhimbili. Lusinde aliitumikia nchi hii kwa moyo wake wote na kwa muda mrefu sana. Amefanya mambo mengi alikuwa Balozi China kwa miaka 10, Balozi Kenya alikaa miaka 10," alisema.

Alisema Lusinde alikuwa akipata matibabu katika hospitali mbalimbali nchini ikiwamo Hospitali ya Benjamin Mkapa iliyoko katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kabla ya kuhamishiwa Muhimbili.

"Bado ndugu tunaambizana na kukusanyika, tutapanga na tutawaarifu lakini mwili wa marehemu utakuja kutoka Dar es Salaam kesho (leo). Mwili ukija tutajitahidi kutafuta chumba cha maiti cha kumweka hadi hapo tutakapomzika," alisema Malecela.

Alisema mazishi ya marehemu yatafanyika baada ya wana ukoo kufika na kukubaliana na baadaye taarifa itatolewa kwa umma kuwa atazikwa wapi na lini.

Malecela alisema Lusinde atakumbukwa kwa utendaji kazi wake uliotukuka na uzalendo kwa nchi yake kupitia nafasi mbalimbali alizotumikia.

"Mimi marehemu (Lusinde) ni kaka yangu nitamkumbuka ni msomi na mimi nilipoingia shuleni, alinifanyia 'encouragement' kubwa sana na hata nilipokwenda kusoma India yeye ndiye nilikuwa nawasiliana naye na wakati mwingine alikuwa ananitumia fedha za matumizi na sasa namkumbuka kwa mapenzi makubwa sana," alisema.

Lusinde alikuwa mmoja wa mawaziri 11 wa kwanza wa Tanganyika na alishika nafasi mbalimbali zikiwamo Serikali za Mitaa (1961-1963), Mambo ya Ndani ya Nchi (1963- 1965), Mwaka 1965-1967 Waziri wa Mawasiliano, Ajira na Kazi (1965-67), na 1974-1975 alihudumu kwenye uwaziri wa Mawasiliano na Ujenzi.

Mwaka 1975 aliteuliwa na Mwalimu Nyerere kuwa Balozi wa Tanzania nchini China. Alihudumu huko hadi Septemba 1984 alipoteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Kenya.



Meneja Mawasiliano wa TBL Plc, Amanda Walter (wa pili kulia), akikabidhi fulana za uhamasishaji kampeni za usalama barabarani kwa Kamishna Msaidizi wa Polisi kutoka Kikosi cha Usalama Barabarani, makao makuu, Mkadam Mkadam, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni maofisa wa jeshi hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majinge achukua fomu urais CHADEMA

**Na Mary Geofrey**

DAKTARI Mayrose Majinge, amekuwa mwanachama wa pili kuchukua fomu ya kuomba ridhaa ya kupeperusha bendera ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwenye uchaguzi wa urais Oktoba, mwaka huu.

Dk. Majinge amekabidhiwa fomu hiyo jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Uchaguzi CHADEMA, Reginald Munisi, katika ofisi za makao makuu ya chama hicho.

Dk. Majinge pia amekuwa mwanamke wa kwanza kwenye chama hicho, kuchukua fomu hiyo tangu shughuli hiyo ianze Julai 4, na inayotarajiwa kuhitimishwa Julai 19, mwaka huu.

Wa kwanza kuchukua fomu hiyo ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, aliyechukua Julai 4, mwaka huu, kupitia wakala wake David Jumbe.

Akizungumza baada ya kuchukua fomu hiyo, Dk. Majinge alitaja mambo kadhaa ambayo atayafanyia kazi endapo atachaguliwa kugombea nafasi hiyo na kupata ridhaa ya wananchi kuwa rais wa Tanzania.

Alisema endapo atapata ridhaa hiyo, atajenga mfumo imara na madhubuti wa uongozi wa taifa, kwa ajili ya maslahi ya kizazi cha sasa na vijavyo.

Alisema pia ni kuwezesha upatikanaji wa katiba ya wananchi na tume huru ya uchaguzi kwa ajili ya kulinda haki na wajibu wa kila Mtanzania, pamoja na kudhibiti utawala wa kibabe.

Dk. Majinege alisema endapo atafanikiwa kuwa Rais wa Tanzania, ataboresha utawala wa sheria kwa kuondoa sheria kandamizi na kuhakikisha taifa lina sheria zinazozingatia haki na utu kwa wote.

Aliahidi pia kuwezesha kila Mtanzania kuwa na uhakika wa chakula na matibabu, kupata elimu yenye kujenga maarifa na uwezo mkubwa wa kufikiri ili kutumia fursa zilizopo kuishi kwa uhuru na furaha.

"Nitahakikisha nawezesha uwapo wa ajira kwa mujibu wa kila fani na taaluma ya Mtanzania," aliahidi Dk. Majinge.

Kadhalika, Dk. Majinge alisema ameamua kugombea nafasi hiyo, ili kuboresha mfumo wa madaraja ya mishahara ya wafanyakazi wote wa taasisi za umma na binafsi ili yaweze kukidhi mahitaji ya maisha.

"Nitawezesha mazingira rafiki na yenye maslahi kwa watu wanaoshughulikia kilimo, ufugaji na viwanda. Kuboresha utalii, kuweka mazingira mazuri katika biashara ya madini kwa wazawa na wawekezaji wa nje," alisema Dk. Majinge.

Alihidi kuwawezesha raia wa Tanzania wanaoishi nje ya nchi kuwa na uraia pacha.

"Hizi ni ahadi zangu kwa Watanzania kuhusu mambo ya msingi niliyoyaandaa kwa mujibu wa taaluma yangu. Endapo chama kitanipitisha nawaomba Watanzania wote bila kujali itikadi zetu, watuunge mkono CHADEMA ili kuwezesha ahadi nilizotoa leo ziwe kweli," alisema Dk. Majinge.

## Magufuli ateua DC, ma-DED

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amefanya uteuzi wa mkuu wa wilaya mmoja na wakurugenzi wa halmashauri watano.

Kwa mujibu wa Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Rais Magufuli amemteua Lauteri John Kanoni kuwa Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe.

Kabla ya uteuzi huo, Kanoni alikuwa Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Serikali za Mitaa katika Mkoa wa Songwe, na anachukua nafasi ya Ally Mohammed Kasinge.

Pia Rais Magufuli amemteua Bashir Paul Mhoja kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa mkoani Iringa.

Kabla ya uteuzi huo, Mhoja alikuwa Mwanasheria wa Halmashauri ya Mji wa Geita mkoani Geita na anachukua nafasi ya Robert Mgendi Masunya.

Ramadhan Salmin Possi ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze mkoani Pwani, na kabla ya uteuzi huo, Possi alikuwa Ofisa Mipango katika Jiji la Tanga mkoani Tanga na anachukua nafasi ya Amina Kiwanuka ambaye amestaafu.

Mteule mwingine ni Baraka Michael Zikatimu ambaye anakuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo mkoani Tabora. Kabla ya uteuzi huo, Zikatimu alikuwa Ofisa Mipango katika Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli mkoani Tanga, na anachukua nafasi ya Margareth Jonathan Nakainga, ambaye amestaafu.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa Rais Magufuli amemteua John John Nchimbi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara. Kabla ya uteuzi huo, Nchimbi alikuwa Ofisa Rasilimali Watu katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro mkoani Morogoro.

Kadhalika, Rais Magufuli amemteua Emmanuel Matinyi Johnson kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga. Kabla ya uteuzi huo, Emmanuel Matinyi Johnson alikuwa Ofisa Elimu wa Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa uteuzi wa viongozi hao ulianza jana.

# Jumuiya ya Burunge hifadhi inayosimama kwa mtindo wa serikali, bajeti mabilioni

**Na Salome Kitomari, aliyekuwa BABATI**

***SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilikuwa na simulizi ya kina namna Jumuiya ya Hifadhi za Jamii Burunge ilivyozaliwa, kujiendesha na mafanikio ya juu hadi kufikia ngazi ya kijiji kuwa na mipango, bajeti na akiba, inayofanana na halmashauri zilizopo. Ufuatao ni mwendelezo wa simulizi hiyo:***



Katibu wa Jumuiya ya Hifadhi ya Burunge, Benson Maise, akionyesha moja ya matrekta lililonunuliwa na jumuiya hiyo, kwa ajili ya kulima mashamba ya wananchi na huduma nyingine katika vijiji 10 vinavyomiliki eneo la uhifadhi. **PICHA: SALOME KITOMARI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sangaiwe, Marian Mwanso, anasema wamepata mafanikio makubwa kwa kuwa na miradi ya maendeleo kama nyumba za walimu, ofisi ya kijiji, choo cha ofisi ya kijiji, wamechangia Sh. milioni 20 katika ujenzi wa Shule ya Sekondari Mbugwe na ujenzi wa bwawa ambao wamechangia Sh. milioni 94.

"Uhifadhi umeimarika maana jamii inatambua WMA na tunashirikiana kiasi kwamba hakuna shughuli za kibinadamu kwenye eneo la hifadhi.

"Tuna Hoteli za Tarangire, Simba Lodge na Sangaiwe Tent Lodge. Tumeweka vijana wanakusanya mapato na mwisho wa mwezi makusanyo yanaingia kwenye akaunti ya kijiji na hadi sasa tuna Sh. milioni 500 benki," anasema.

Anabainisha kuwa kati ya fedha hizo, za WMA ni Sh. milioni 103 na Sh. milioni 400 zimetokana na mapato ya hoteli mbili zinazomilikiwa na kijiji, moja ina miaka miwili na nyingine miaka minne.

"Miradi iliyopo kwenye mpango wa kutumia hizo Sh. milioni 500 ni kujenga vibanda kwa ajili ya uhakiki wa wageni kabla hawajaingia hotelini, ujenzi wa zahanati (Sh. milioni 84), maji, ujenzi wa madarasa mawili na ofisi. Miradi yote tuliyopanga ina fedha za kuitekeleza, hatupangi halafu ndiyo tukatafute fedha," anasema.

Anasema mipango ya miradi ya kipaumbele inaibuliwa na wananchi kwenye mkutano wa kijiji.

"Nimekuwa kiongozi kabla ya kuanzishwa kwa WMA. Kabla ya WMA, michango ilikuwa kero kubwa, wananchi walishindwa kulala nyumbani na wengine kukimbia kijiji, lakini kwa sasa wamerudi na amani imetawala kwa kuwa hakuna kero," anasema.

Kiongozi huyo anakitaja kikwazo kilichoko katika eneo lake ni tembo kuvamia na kuharibu mazao pamoja na simba kutaka kushambulia wanyama na kuvamia binadamu, lakini wanadhibitiwa. Anasema pundamilia pia wamekuwa sehemu ya vikwazo hivyo kutokana na kuharibu mazao na si wanyama walioko kwenye orodha ya fidia.

Mjumbe wa Serikali ya Kijiji, Juliana Makseli, anasema manufaa ya WMA ni makubwa kwa kuwa watoto wao wanasoma kwa raha na walimu wana mahali pa kuishi.

"Jamii kwa sasa haihangaiki na michango. Inapotokea, kijiji kinajua kifanyeje kupeleka na si wananchi kuchangishwa fedha," anasema.

### KUSOMESHA WASIOJIWEZA

Makseli pia anabainisha kuwa kijiji huangalia watoto yatima na wanaotoka katika familia zisizojiweza kiuchumi na kuwasomesha.

"Tumeweka utaratibu wa kusaidia wanafunzi waliofaulu kwenda vyuo vikuu. Kila mwaka tunatenga Sh. milioni tano wanagawana kulingana na idadi yao, hii ni namna ya kuwatia moyo watoto wetu kusoma kwa bidii hadi vyuo vikuu," anasema.

Anabainisha kuwa wapo vijana wanaosomeshwa na kijiji hicho katika vyuo vya ufundi na pia kumekuwa na utaratibu wa kusaidia kaya maskini zikiwamo za wajane.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Olasiti, Daudi Milengori, anasema WMA imesaidia maendeleo ya kijiji chake, akitolea mfano Shule ya Msingi Eluway ambayo kumejengwa madarasa matano, matundu 24 ya vyoo na nyumba ya walimu wawili.

Anasema kuwa katika Shule ya Msingi Urudukai, wamejenga nyumba mbili za walimu, madarasa mawili na ofisi ya walimu, matundi 24 ya choo, madawati 40 bila mchango wa wananchi, huku wakijenga darasa moja kwa ajili ya shule ya sekondari iliyoko karibu na kijiji hicho.

"Fedha zinapokuja, tunaongozwa na bajeti iliyoandaliwa na halmashauri ya kijiji, inapelekwa kwenye mkutano wa kijiji unaoangalia vipaumbele. Kijiji chetu kipaumbele ni elimu na ndiyo maana tunajenga miundombinu ya elimu," anasema.

### MZEE WA MICHANGO

"Ninajisikia vizuri sana, nimekuwa mwenyekiti wa kijiji kwa muda mrefu, kipindi cha michango niliwapelekesha sana kuhakikisha fedha zinapatikana mpaka nikaitwa 'mzee wa michango' na uchaguzi uliopokuja hawakunichagua tena.

"Baada ya miaka mitano wananchi walinichagua baada ya kujua kumbe sikuwa mzee wa michango bali hatukuwa na fedha na ilikuwa lazima kurudi kwenye mifuko ya wananchi ili tufanye miradi ya maendeleo.

"Baada ya kuongozwa na mwingine, walinikumbuka na kunichagua awamu ya kwanza na pili na walipoona ninasimamia vizuri miradi ya maendeleo wamenichagua tena kwa awamu ya tatu. Kwa sasa, ninalala usingizi, sina kero kwa wananchi," alisifu.

Betuel Thomas, mjumbe Kamati Maalum ya Mazingira (AA) katika Kijiji cha Vilimavitatu, anasema WMA imewaletea maendeleo na wamejenga sekondari ya kidato cha tano na sita, zahanati na shule ya msingi na zote ni za kisasa.

> **"Tumeweka utaratibu wa kusaidia wanafunzi waliofaulu kwenda vyuo vikuu. Kila mwaka tunatenga Sh. milioni tano wanagawana kulingana na idadi yao, hii ni namna ya kuwatia moyo watoto wetu kusoma kwa bidii hadi vyuo vikuu," anasema.**

"Wawekezaji wameajiri zaidi ya vijana 300 na ni wenye familia, huwezi kutembea hatua tano hujakutana na mtu aliyenufaika na WMA, tunalinda maliasili yetu bila woga," anasema.

Makamu Mwenyekiti wa WMA, Emmanuela Willium, anasema jumuiya hufuatilia kwa karibu utunzaji wa mazingira na vijiji vinavyoshindwa kufikia malengo, huadhibiwa kwa fedha kuzuiwa hadi watakaporekebisha kasoro.

### KAULI YA SERIKALI

Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Babati, Hamisi Malinga, aliiambia Nipashe Mei 23 mwaka huu kuwa, halmashauri inashirikiana na vijiji kulinda shoroba ya Tarangire na Manyara kwa kuwa ni muhimu kwa uhifadhi.

"Eneo la Manyara kuna udongo wenye madini muhimu kwa ajili ya nyumbu, lazima tushirikiane na WMA kutunza eneo hili," alisema.

Alisema kuwa mwaka 2004 hadi 2006, WMA iliundwa na vijiji vitano na baadaye vilifikia 10 kwa kila kimoja kutoa eneo ili kuunda hifadhi.

Alisema vijiji hivyo vimejitegemea kwa kutekeleza miradi ya maendeleo kulingana na vipaumbele vyao na kumetoa unafuu mkubwa kwa halmashauri.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, upatikanaji wa fedha umetoa ahueni kwa halmashauri kwa kuwa zaidi ya Sh. milioni 100 hupelekwa kwenye kila kijiji kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka WMA badala ya kutolewa na serikali.

"Imesaidia sana maana sasa wanafanya miradi wenyewe na serikali inapeleka nguvu kwingine. Kama kusingekuwa na WMA, halmashauri ilitakiwa kupeleka fedha na tungepeleka kidogo kutokana na uhaba wa rasilimali.

"WMA ni eneo muhimu sana, linapaswa kulindwa. Kuna hoteli 17 za kitalii zinazoingiza fedha nyingi, ni ya pili kimapato baada ya Serengeti inayokusanya Sh. bilioni 2.7. WMA nyingi kwa sasa zimekufa, lakini hii imeendelea kuwapo," alisema.

Alisema uhifadhi umesaidia na faida zake zimeonekana kwenye ikolojia na kiuchumi ambazo zimeongeza uwezo wa halmashauri kuhudumia na kuna fedha halmashauri inapata zinaingia mfuko mkuu kwa ajili ya kutekeleza shughuli za halmashauri. Malinga alifariki dunia Juni 4 mwaka huu.

ITAENDELEA KESHO

HABARI KITAIFA

# Mtoto anusurika kuuawa na fisi

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

MTOTO anayefahamika kwa jina la Abel Kimbui (13), anayesoma darasa la tano, mkazi wa Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, amenusurika kifo baada ya kung'atwa na fisi shingoni wakati akicheza na wenzake.

Ndugu wa karibu na familia hiyo, Elias Madoshi, ambaye pia ni mchungaji wa kanisa la Free Pentecoste Church mjini Shinyanga, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya jioni, wakati mtoto huyo anayesoma katika Shule ya Msingi Ushirika akicheza na wenzake ndipo walipovamiwa na fisi na kuanza kushambuliwa.

Alisema baada ya fisi huyo kuwavamia, wenzake walikimbia huku yeye akirukiwa kichwani kisha kung'watwa shingoni, lakini baada ya kelele kuzidi fisi huyo alikimbia.

Alisema mtoto huyo alikimbizwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

"Matukio haya ya watoto kung'watwa na fisi katika Manispaa yetu ya Shinyanga yamekithiri sana, hivyo tunaomba mamlaka husika ifanye kazi ya kuwaondoa fisi hawa hapa mjini kwani watamaliza watoto wetu," aliongeza.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga, Rose Malisa, alithibitisha kumpokea mtoto huyo hospitalini hapo, na kubainisha kuwa walimpatia rufani ya kwenda kutibiwa Bugando jijini Mwanza, na kwamba amewasiliana na madaktari wakamweleza kuwa hali yake inaendelea vizuri.

## H/shauri zatumia mil. 81/- kwa posho

Na Sara Magesa, GEITA

HALMASHAURI sita za mkoa wa Geita zimetumia kiasi cha Sh. milioni 81 kwa mwaka wa fedha 2019/20 kama posho kwa watumishi wa idara ya ardhi waliokuwa wakilazimika kupeleka nyaraka za ardhi ofisi ya kamishna wa ardhi Mwanza kutokana na mkoa wa Geita kutokuwapo.

Sasa halmashauri zitaweza kuokoa fedha hizo na kuziingiza kwenye miradi ya maendeleo baada ya serikali kufungua ofisi ya kamishna wa ardhi msaidizi mjini Geita.

Akifungua ofisi hiyo pamoja na kutoa hati miliki 168 kwa wananchi Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema serikali imefungua ofisi hiyo ili kuwaondolea kero wananchi waliolazimika kusafiri hadi mkoani Mwanza kuchukua hati miliki za viwanja vyao.

Aidha, Waziri Lukuvi aliwaagiza makamishna wa ardhi kote nchini kutohuisha upya hatimiliki za viwanja vyenye miaka 33 na kuendelea ambavyo hadi sasa havijaendelezwa.

Lukuvi amewataka kuvirejesha serikali ili ikimpendeza Rais avitoe kwa wananchi wengine wenye nia ya dhati ya kuviendeleza kwa wakati.

"Pekueni hati zote ambazo wamiliki watafika kwa ajili ya kuzihuisha ili waongezewe muda hakikisheni hivyo viwanja kama hawajaendeleza msiongeze muda virudisheni kwa wale waliovienedeleza huisheni muwamilikishe upya kwa miaka mingine 99, na siyo ile 33 ya awali," alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa waziri huyo, Mkoa wa Geita umepima viwanja 41,715 na vyenye hati ni 5,485 na kuwataka makamishna wa ardhi kuwatambua watu 36,230 ambao wanamiliki viwanja vilivyopimwa na hawajachukua hatimiliki.

"Andaeni hati za malipo muwapelekee wote waliopimiwa viwanja na walipe ndani ya siku 90 suala la kuchukua hatimiliki ni la lazima, hakuna sababu ya kuwa kwenye viwanja vilivyopimwa na huna hatimiliki," alisema Lukuvi.

## DC abaini madudu ujenzi wa hospitali

Na Welingtone Masele, TABORA

MKUU wa Wilaya ya Tabora, Komanya Kitwala, ametembelea mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo unaotekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5 na kubaini kasoro za kiufundi.

Akiwa katika mradi huo unaojengwa kwa mfumo wa 'force account' na makandarasi wa ndani eneo la Inala, Kata ya Mpera Manispaa ya Tabora, Kitwala alisikitishwa na mpangilio wa kazi usioridhisha ikiwamo baadhi ya maeneo kutojengwa vizuri.

Kutokana na kasoro hizo, aliagiza kufumuliwa maeneo yote yaliyojengwa chini ya kiwango kuanzia kwenye msingi na kujengwa upya kwa gharama za makandarasi.

Mtaalamu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) mkoani hapa, Goodluck Sanga, aliyeambatana na Mkuu wa Wilaya, alibainisha wazi kuwa msingi wa mradi huo haujajengwa kwa ubora unaotakiwa, hivyo unatakiwa kujengwa upya.

Alisisitiza kuwa ramani ya mradi haijafuatwa ipasavyo kuanzia ujenzi wa msingi jambo ambalo litahatarisha uimara wa kuta za majengo na kuongeza kuwa hata ukubwa wa nondo zilizopo kwenye mchoro sizo zilizotumika.

Sanga alisema sifa ya mkandarasi mzuri ni kutafsiri kwa vitendo mchoro wa kazi anayoifanya na kuhakikisha kila kilichoainishwa katika ramani yake kinafanyiwa kazi kama kilivyo na si kufanya vinginevyo.

Fundi anayesimamia ujenzi wa mradi huo, Mashaka Silika, alimhakikishia Mkuu wa Wilaya kuwa atafanyia kazi ushauri waliopewa ikiwamo kurekebisha kasoro zilizoonekana.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), William Erio, akiangalia huduma mbalimbali zinazotolewa kwa wananchi ikiwamo jinsi mifumo ya TEHAMA inavyorahisisha upatikanaji wa taarifa za michango kwa wanachama wa shirika hilo, alipotembelea banda la mashirikiano la NSSF na PSSSF, katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa Uwanja wa Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: NSSF**

# Erio aridhishwa na huduma banda la NSSF

Na Mwandishi Wetu

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), William Erio, amefurahishwa na huduma mbalimbali zinazotolewa kwa wananchi wanaotembelea banda la NSSF katika Maonyesho ya 44 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba).

Erio alitembelea jana banda la ushirikiano kati ya NSSF na PSSSF na kushuhudia wananchi mbalimbali waliotembelea banda hilo namba 13 wanavyopatiwa huduma kwa haraka.

Miongoni mwa huduma hizo ni pamoja na wananchi kujiunga na NSSF kupitia Mfumo wa Taifa wa sekta isiyo rasmi na kupewa kadi za uanachama papo hapo.

Huduma nyingine zinazotolewa na NSSF kwa wanachama wanaotembelea banda hilo ni taarifa za michango yao inayowasilishwa na waajiri wao kama ni sahihi.

Kadhalika, wananchi na wanachama wanapata elimu kuhusu mafao mbalimbali yanayotolewa na NSSF; Ikiwa ni pamoja na namna wanavyoweza kupanga au kununua nyumba za Kijichi kupitia mpango wa mnunuzi mpangaji.

Vile vile, Mkurugenzi Mkuu alishuhudia namna mifumo ya Tehama inavyomuondolea usumbufu mwanachama wa NSSF ambao sasa halazimiki kufuata huduma kwenye ofisi za Shirika hilo badala yake anaweza kuona taarifa zake kupitia simu yake ya kiganjani.

Kutokana na maboresho hayo ya mifumo mwanachama anaweza kuona taarifa zake kupitia kompyuta mpakato au tovuti ya Shirika ambayo ni www.nssf.or.tz.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# WMA nyingine sasa zikajifunze Burunge

JUMUIYA ya Hifadhi ya Jamii ya Burunge (Wildlife Management Area), iliyopo wilayani Babati, mkoani Manyara, ni ya mfano kwa kuonyesha kuwa, iwapo jamii itaungana na kutunza maeneo kwa malengo mahususi, itafanikiwa kufanya maendeleo makubwa.

WMA hiyo inaundwa na vijiji 10 vilivyopo kwenye kata tatu ambavyo vilitoa maeneo yao na kuunda Jumuiya lenye ukubwa wa kilomita za mraba 283 ambayo hutumia eneo hilo kwa uhifadhi na kuvutia watalii.

Mapato ya Jumuiya hiyo kwa mwaka 2017/2018 yalikuwa Sh. bilioni 2.7,ambazo kwa mujibu wa kanuni za uendeshaji wa WMA, asilimia 70 ilibaki kwa Jumuiya, asilimia 20 Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori (TAWA) na asilimia 10 halmshauri.

Kutokana na mgawanyo huo, kila kijiji kilipata Sh. milioni 100.9, ambazo ana hiyari ya kuzigawanya kwenye shughuli za maendeleo kulingana na vipaumbele vyao.

Aidha, mabadiliko ya kanuni yalifanyika mwaka 2018/2019, na mwaka huu WMA zilipata Sh. bilioni 2.5 ambazo ziligawanywa kwa asilimia 65 kubaki kwenye Jumuiya, asilimia 25 inakwenda TAWA na asilimia 10 zinakwenda halmashauri.

Hifadhi hiyo iko katikati ya hifadhi za Taifa za Tarangire na Ziwa Manyara, ambazo zina njia ya kupita wanyama ijulikanayo kama shoroba, ambayo huwawezesha wanyama kwenda eneo jingine kutafuta mahitaji ya miili yao.

Katika eneo hilo kuna wawekezaji sita waliojenga hoteli za kitalii, kuna eneo la utalii wa picha na shughuli nyingine ambazo huingiza kipato.

Kutokana na fedha hizo vijiji vimetekeleza miradi ya huduma za jamii kama ujenzi wa miundombinu ya shule, nyumba za walimu, zahanati, maji na huduma nyingine za kijamii ambazo zinanufaisha jamii husika.

Kati ya vijiji 10 kimoja kinamiliki hoteli mbili za kitalii ambazo hupokea wageni na kuwawezesha kupata zaidi ya Sh. milioni 400 kwa mwaka na wakichanganya na mgawo kutoka WMA na kuwafanya kuwa na jumla ya Sh. milioni 500 zinazosubiri kupangiwa matumizi.

Burunge ni WMA ya mfano kwa kuwa ni kati ya 38 zilizopo nchini, na 16 ndiyo zinafanyakazi huku nne zikifanya vizuri kwenye kutunza maeneo na kupata fedha ambazo hugawanywa kwenye vijiji wanachama.

Kama Jumuiya zote zingeiga kinachofanywa Burunge ni wazi kuwa TAWA na halmashauri zingepata fedha nyingi ambazo moja kwa moja zingechangia maendeleo ya wananchi na pato la taifa kwa ujumla.

Katika vijiji vyote 10, msamiati wa michango kwa ajili ya maendeleo ya jamii umesahaulika badala yake anabuni miradi ya kutekeza kwa fedha walizonazo, na wengine wamekwenda mbali zaidi kwa kusomesha watoto kutoka familia duni ambao wamesomeshwa hadi elimu ya juu.

Pia, wananchi wametoa ajira kuanzia ndani ya Jumuiya na kwenye hoteli za wawekezaji, na kwa sasa maisha ya eneo hilo yameboreka kwa kiasi kikubwa.


Ni wazi kuwa kinachofanyika Burunge ni jibu la utatuzi wa matatizo ya jamii zinazoshi jirani na hifadhi za Taifa za maeneo yaliyohifadhiwa, na sasa ni vyema WMA nyingine zikaiga na kuchukua hatua kuhakikisha wanazisimamia vyema na kujiletea maendeleo yao na kutoa mchango kwa taifa.

Kama kijiji kinapata Sh. milioni 100 kutokana na uhifadhi maana yake vijiji vilivyopo kwenye WMA 38 vinaweza kuleta mabadiliko makubwa, na kila halmashauri ikawa na uhakika wa mapato na hazihangaiki kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza huduma za jamii kwenye kata au vijiji.

Hakuna ubishi kuwa keki ya taifa haitoshi kugawa kila mahali, lakini kunapokuwa na mahali panaweza kutengeneza fedha nyingi, sisi tunaona ni vyema pakatumiwa vizuri ili kuinua maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Uchaguzi mkuu Malawi umekuja na funzo hili

Na Sabato Kasika

MWAKA 1994 ulikuwa mwisho wa utawala wa miaka 30 wa chama kimoja cha Malawi Congress Party (MCP) cha Rais wa kwanza, Dk. Haustings Kamuzu Banda baada ya uchaguzi ndani ya mfumo wa vyama vingi.

Katika uchaguzi huo, Chama cha United Democratic (UDF) cha Bakili Muluzi, kiliibuka na ushindi, ambapo tangu wakati huo, MCP imeendelea kuwekwa pembeni hadi hivi karibuni ilipoibukia kwa kishindo.

Chama hicho kilicholeta uhuru wa Malawi mwaka 1964 kiliwekwa pembeni baada ya kutawala miaka 30. Kilitupwa nje kwa miaka 26 hadi uchaguzi wa hivi karibuni, ambao umekiwezesha kurudi madarakani kwa mara nyingine tangu walipokiondoa mwaka 1994.

Kimsingi wananchi wa Malawi walikuwa na sababu za kukiweka pembeni chama hicho, kutokana na uongozi wa mwanzilishi wake, Dk Banda, kwenda kinyume na matarajio yao.

Historia inaonyesha kuwa kiongozi huyo aligeuka kuwa kibaraka wa Wazungu na kuwacha viongozi wenzake wa Afrika na pia kugawa wananchi wake na hivyo kusababisha matabaka na utengano.

Vitendo hivyo na vingine vingi vilisababisha yeye na chama chake kuchukiwa hadi kufikia kukiondoa madarakani kwa njia ya kura ingawa sasa kimerudi upya kutawala nchi hiyo kikiwa chini ya Rais Lazarus Chakwera.

Kitendo cha wananchi wa Malawi kukirudisha chama hicho madarakani, ni wazi kwamba, hata vyama vya upinzani barani Afrika vina la kujifunza kutokana kile wapigakura walichokifanya.

Jambo la kujifunza ni kwamba, kwa nyakati tofauti, vyama vya upinzani vimepewa ridhaa kuongoza nchi hiyo, lakini wananchi wameamua kukirudisha kinara wa uhuru.

Hivyo wapinzani nchini na Afrika wanatakiwa kujifunza kwa yale yalitokea Malawi ili wanapotafuta ridhaa ya kuongoza nchi, wasifanye makosa yatakayoleta kutimuliwa.

Hapa maana yake ni kwamba, chama kilicholeta uhuru kimejifunza kutokana na makosa na kujirekebisha, kisha kikaomba tena ridhaa kwa wananchi nao wakaamua kukipa kibali cha kuiongoza nchi.

Mbali na hilo, yawezekana kuna udhaifu uliofanywa na vyama ambavyo viliwahi kutawala nchi hiyo na kusababisha MCP kupata upenyo wa kukiwezesha kujenga na hatimaye kupata ushindi.

Hivyo wakati upinzani ukimimina salamu za kumpongeza rais mpya wa nchi hiyo kwa ushindi, ni vyema pia wakawa na la kujifunza hasa kile kilichokirudisha chama tawala madarakani baada ya kukaa nje kwa miaka 26.

Yawezekana wananchi wa Malawi wameona ndani ya vyama vyote ambavyo vimewahi kuiongoza nchi hiyo tangu mwaka 1994, hakuna lolote, ndipo wakaamua kurudi kwenye chama chao cha zamani.

Baadhi ya watu wanaweza kudhani kwamba chama ambacho kimeshinda uchaguzi wa Malawi ni kipya, lakini ukweli ni kwamba ni kikongwe kilicholeta uhuru wa nchi hiyo.

Kwa kawaida chama kikishindwa katika uchaguzi, kinakuwa cha upinzani huku kilichoshinda kikiwa ni chama tawala, hivyo hata MCP kilikuwa tawala, kisha cha upinzani baada ya kushindwa na sasa ni chama tawala.

MCP inarudi madarakani kurekebisha changamoto zilizofanywa na viongozi waliowahi kuiongoza nchi hiyo tangu upinzani uliposhinda uchaguzi mkuu wa mwaka 1994.

Siyo vibaya kujifunza kwa vyama vingine ambavyo vilifanikiwa kupata ushindi na sasa vinaendelea kuongoza nchi, na wananchi wanaendelea kuviamini bila kujali kwamba kulikuwa na chama kilicholeta uhuru.

Kwa mfano tangu kuangushwa kwa chama cha kijamaa kilicholeta uhuru wa Zambia cha United National Independence Party (UNIP) tangu mwaka 1991 cha Baba wa Taifa Dk. Kenneth Kaunda, hadi leo kiko pembeni, kwa miaka takribani 30 .

Kutofurukuta kwa chama cha Kaunda ni wazi vyama mbalimbali ambavyo vimekuwa vikishinda uchaguzi mkuu wa Zambia kwa nyakati tofauti vinafanya kile ambacho Wazambia wanakitaka.

Kwa hiyo wapinzani na vyama tawala Afrika wafahamu kuwa kitokea wakishika madaraka, kuna uwezekano wa kushindwa iwapo watakwenda kinyume na matarajio ya wapigakura.

MAKALA MAALUM

KABLA SHAHADA UZAMILI...

# Prof. Nombo: TIA tumekusanya PhD 13 na nyingine 29 zinakuja

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Uhasibu Tanzania (TIA), ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, ulioanzishwa rasmi Julai Mosi 2002, ukichukua nafasi ya kilichokuwa Chuo cha Uhasibu Dar es Salaam (DSA) ikiwa ni sehemu ya mpango wa maboresho ya taasisi za umma nchini.

Katika kutimiza azma ya kuwafikia wananchi kwa urahisi, taasisi hiyo ina kampasi sita ambazo ni Dar es Salaam (makao makuu), Mbeya, Singida, Mtwara, Mwanza na Kigoma.

Mkuu wa TIA, Profesa Caroline Nombo anasema kuwa majukumu makuu ya taasisi hiyo ni kutoa mafunzo, ushauri wa kitaalamu na kufanya utafiti kwenye nyanja za uhasibu, ununuzi na ugavi pamoja na maeneo mengine ya kibiashara. Pia kuzalisha mapato ili kukidhi angalau asilimia 50 ya bajeti yake kwa lengo la kujitegemea siku zijazo.

Profesa Nombo anasema kuwa katika miaka mitano ya awamu hii ya uongozi wa serikali, taasisi imepata mafanikio katika maeneo makuu manne ambayo ni: Mafunzo; ushauri na utafiti; miundombinu na ongezeko la udahili; na maendeleo ya wafanyakazi.

Katika eneo la mafunzo, Profesa Nombo anasema kwa kuzingatia elimu ni moja ya vipaumbele vya serikali ya awamu ya tano, TIA iliweka mikakati ya kuendana na kasi ya serikali kwa kuzalisha wanataaluma bora katika fani za uhasibu, ununuzi na ugavi, usimamizi wa biashara, uongozi wa rasilimali watu, masoko na uhusiano wa umma pamoja na uhasibu wa umma na fedha.

Anasema kwa kutambua umuhimu wa fani hizo katika dhana nzima ya viwanda, taasisi ilipitia upya mitaala ya kozi zote kuanzia ngazi ya cheti, stashahada, shahada na stashahada ya uzamili, upitiaji ukianza mwaka 2015/16 na unaendelea hadi sasa.

"Kuboreshwa kwa mitaala kumewapatia ujasiri wahitimu na kuwaongezea uwezo wa kujiajiri, hivyo kutoa fursa ya ajira kwa Watanzania wengine.

"Vilevile, tumeandaa mitaala mipya ambayo itaanzishwa hivi karibuni kwa lengo la kukidhi mahitaji ya soko la ajira, ili kuchochea mabadiliko katika maendeleo ya nchi," anasema.

Katika eneo la ushauri na utafiti, kiongozi huyo wa taasisi anasema kuwa, kutokana na msukumo wa serikali kusisitiza mamlaka za serikali kuu na serikali za mitaa kufanya kazi kwa ufanisi na kukusanya mapato, tangu mwaka 2015/16 hadi sasa, taasisi imefanya utafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kuendesha mafunzo kwa mamlaka za serikali za mitaa, halmashauri na taasisi nyinginezo.




Mwonekano wa jengo la utawala na taaluma la TIA Kampasi ya Dar es Salaam.

Alisema mafunzo yalijikita katika uibuaji na uthamini wa vyanzo vya mapato, mbinu bora za ukusanyaji na usimamizi wa mapato, uandishi wa miradi ya kimkakati yenye kuchochea mapato endelevu, ushirikishwaji wa vijana katika dhana nzima ya uchumi wa viwanda, uandishi bora wa vitabu na ufungaji wa hesabu kwa kuzingatia Viwango na Miongozo ya Uhasibu wa Umma wa Kimataifa (IPSAS).

"Mafanikio mengine katika eneo hili ni utambuzi wa mali na uandishi wa daftari la mali kwa kuzingatia Mwongozo wa Serikali wa Mwaka 2019.

"Mengine ni usimamizi na utekelezaji wa mikataba mbalimbali, taratibu za ununuzi wa umma kwa kuzingatia miongozo pamoja na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na mabadiliko yake ya mwaka 2016.

"Baadhi ya halmashauri na taasisi tulizofanya nazo kazi ni pamoja na Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Halmashauri ya Wilaya ya Busekelo, Halmashauri ya Manispaa ya Songea na Chama cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu (CHAKAMWATA)," anasema.

Kwenye eneo la miundombinu na udahili, Profesa Nombo anasema kutokana na mpango wa serikali wa kutoa elimumsingi bila malipo, Watanzania wengi wamepata fursa ya kusoma, hivyo kuwapo ongezeko kubwa la wahitimu wa kidato cha nne, ambao miongoni mwao wana uhitaji wa kujiunga na kozi za cheti cha awali zinazotolewa na TIA.

Anabainisha kuwa mwaka jana, taasisi ilipokea wanafunzi 5,300 katika kampasi zake sita kujiunga na kozi mbalimbali za cheti cha awali ambao walipangwa na serikali moja kwa moja kupitia Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

"Kwa ujumla ongezeko hili imekuwa fursa kubwa kwa taasisi, kwani licha ya ushindani uliopo, idadi ya udahili katika kampasi zote imeongezeka kwa asilimia 44 kutoka 8,781 mwaka 2014/15 hadi 12,616 mwaka 2019/20, huku idadi ya wanafunzi katika kampasi zote sita ikiongezeka kwa asilimia 32 kutoka 14,985 mwaka 2014/15 hadi 19,771 mwaka 2019/20," anafafanua.

Anasema katika kuunga mkono jitihada hizo za serikali, taasisi imefanikiwa kuongeza idadi ya wahadhiri, sambamba na kufanya maboresho ya miundombinu iliyokuwapo na kuongeza miundombinu mipya ya madarasa, kumbi za mihadhara, maktaba, maabara za kompyuta, mabweni na mabwalo ya chakula.

Kutokana na ongezeko hilo la wanafunzi, Proefsa Nombo anasema kuwa, taasisi sasa inatekeleza miradi ya ujenzi wa jengo la taaluma lenye kumbi mbili za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 922 kwa wakati mmoja, madarasa 12 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,920, maabara ya kisasa ya kompyuta yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 408 na maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja.

Vilevile, anasema wanaendelea na mradi wa ukarabati wa majengo mbalimbali katika Kampasi ya Dar es Salam, ujenzi wa ukumbi wa mihadhara na ukarabati wa jengo la utawala katika Kampasi ya Mbeya, Ujenzi wa Maktaba na Maabara ya Kompyuta, marekebisho ya madarasa katika Kampasi ya Singida pamoja na ujenzi wa bwalo katika Kampasi ya Mtwara.

Kuhusu maendeleo ya wafanyakazi, Profesa Nombo anasema kuwa, taasisi imekuwa pia ikisisitiza kufanya kazi na kutoa huduma kwa wananchi kwa weledi.

Kama sehemu ya utekelezaji wa dira yake inayotaka kuwa taasisi yenye ufanisi katika kutoa huduma bora za elimu, utafiti na ushauri kwa jamii, Profesa Nombo anasema TIA imejikita pia katika kuwaendeleza wafanyakazi, akibainisha kuwa mwaka tangu 2015/16 hadi sasa, taasisi imewaendeleza watumishi 13 kwenye mafunzo ya shahada ya uzamili, na wahadhiri 29 kwenye shahada ya uzamivu (PhD).

"Mpaka sasa, taasisi ina jumla ya wahadhiri 13 ambao wana PhD kwenye fani mbalimbali. Hii ni hatua kubwa kwa taasisi ukilinganisha na hali ilivyokuwa awali. Kutokana na kuwapo idadi ya wahadhiri wenye ngazi ya PhD, taasisi inategemea kuanza kutoa mafunzo ngazi ya shahada ya uzamili katika mwaka ujao wa masomo.

"Hatua hii ni muhimu kwa taasisi kwa kuwa itaongeza idadi ya wanachuo wanaodahiliwa kila mwaka, pia itaongeza wigo wa elimu kwa wananchi katika ngazi hiyo.

"Hatua zote hizi zinachukuliwa ili kuhakikisha TIA inaendelea kutoa mchango katika soko la ajira kwa kutoa wahitimu wenye viwango na ubora unaohitajika ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuchochea mabadiliko ya uchumi wa viwanda, lakini kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani na kupunguza utegemezi kwa serikali," anasema.

Profesa Nombo anasema taasisi imejipanga kuendelea kutoa wahitimu wenye kuongeza tija katika sehemu zao za kazi na wenye uwezo wa kujiajiri ili kuleta mabadiliko chanya kwa taifa.

"Pia, taasisi imejipanga kuendelea kutoa ushauri na kufanya utafiti kwenye nyanja za uhasibu, ugavi na nyanja nyingine za biashara, unaolenga kutatua matatizo ambayo nchi inakabiliana nayo kuelekea uchumi wa viwanda," anasema.



Kumbi za mihadhara za TIA Kampasi ya Singida.

HABARI PICHANI

# MAONYESHO YA 44 YA BIASHARA YA KIMATAIFA DAR ES SALAAM



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Tigo, Simon Karikari (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Nancy Lyimo ambaye ni Msimamizi wa Banda la kampuni hiyo, alipotembelea katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa katika uwanja wa Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Tigo, Kanda ya Pwani, Joseph Mutalemwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Daktari wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Lawanna Msiliwova (kulia), akitoa maelezo kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya afya ya binadamu katika banda la hospitali hiyo. **PICHA: ANTHONY SIAME**




Wananchi wakiangalia gari linalotumia mafuta na gesi asilia katika Banda la Chuo cha Ufundi na Teknolojia cha Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Wananchi waliotembelea Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam wakipata huduma kupitia mashine za ATM, kwenye banda la NMB. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Wananchi wakiwa kwenye msururu mrefu kusubiri kuingia kwenye viwanja vya maonyesho hayo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**



Mkurugenzi wa Matango Cashewnut wasindikaji wa bidhaa za korosho, Tatu Msatango (kushoto), akionyesha korosho kwa wananchi waliotembelea banda la wajasiriamali katika maonyesho hayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

HABARI KITAIFA

# Wadau waombwa ujenzi vyoo vya kisasa shuleni

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, amewaomba wadau wa maendeleo wilayani humo kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali ili kuwezesha kujengwa vyoo bora na vya kisasa kwenye shule za sekondari na msingi ili wanafunzi hususani wa kike wajisitiri kwenye vyoo safi na salama.

Alisema hayo wakati wa uzinduzi wa choo cha kisasa kilichojengwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro katika Shule ya Sekondari Tubuyu Kata ya Boma kwa ajili ya mtoto wa kike.

Alisema wadau hao wamekuwa nguzo kubwa kwa serikali baada ya kuridhishwa na usimamizi mzuri wa fedha na miradi inayotekelezwa.

Alilipongeza Baraza la Madiwani lililomaliza muda wake na Mkurugenzi wa Manispaa hiyo kwa kubuni na kusimamia mradi huo, huku akitaka usiishie hapo bali uendelee katika shule zingine ili ziwe na vyoo vyenye hadhi hiyo lengo kumhifadhi mtoto wa kike.

" Serikali imefanya mambo makubwa ikiwamo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara , hospitali za kisasa, vituo vya afya vya kisasa, ununuzi wa ndege, ujenzi wa reli ya kisasa na ujenzi wa bwawa kubwa la kufua umeme la Julius Nyerere," alisema Msulwa.

Alitaka Manispaa ya Morogoro kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa vyoo bora kwenye shule kutokana na kuwapo kwa mahitaji makubwa katika shule hizo," alisema.

"Tatizo la vyoo katika shule zetu ni kubwa sana kwa kuwa watoto ni wengi na matundu ya vyoo ni machache, hivyo niagize Manispaa kwa kushirikiana na wadau wengine waliopo katika Wilaya ya Morogoro kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali ili watoto wetu wajisitiri katika vyoo safi na salama," alisema Msulwa.

Aliwataka wanafunzi wa shule ya sekondari Tubuyu kuongeza bidii katika masomo na kujiepusha na tamaa ili ndoto zao za kupata mafanikio ya kimaendeleo ziweze kutimia.


Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Sheilla Lukuba, alisema utafiti mbalimbali umefanyika kuhusiana na sababu za mahudhurio hafifu ya mtoto wa kike darasani kutokana na vyoo visivyofaa kwa matumizi hasa kwa watoto wa kike.

"Tutaendelea kushirikiana na wadau, lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba tunaunga mkono juhudi zozote zile ambazo zinaondoa umaskini wa Mtanzania au mwananchi wa kawaida pamoja na kuwaondolea adha wanafunzi wa kike wanapoingia katika hedhi," alisema Lukuba.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Tubuyu, John Mniko, alisema shule ina jumla ya wanafunzi 409 kati ya hao wavulana 190 na wasichana 219, na choo kilichojengwa cha wanafunzi wa kike kina jumla ya matundu ya choo 12 ikiwamo moja kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu na kimegharimu Sh. milioni 35 zilizotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa hiyo.

Nao baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo wakizungumza kwa nyakati tofauti shuleni hapo waliishukuru serikali na manispaa hiyo kwa kuwajengea choo cha kisasa ambacho wengi wao hawajawahi kukiona, na kuahidi watakitunza huku wakiomba kuongezewa kingine.

.



Mifugo ikitafuta chakula kwenye rundo la takataka zilizotelekezwa bila ya kuzolewa kwa muda mrefu katika eneo la Tabata Bonyokwa kwa Mahita, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kompyuta zaibwa kimaajabu shuleni

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WATU wasiojulikana wameiba kompyuta 16 na vifaa vingine vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 24.2 katika shule inayoendelea kujengwa ya Sheikh Idrissa Abdul Wakili, iliyopo Kizimbani mjini Wete kisiwani Pemba.

Kompyuta hizo, zinadaiwa kuibwa katika mazingira tata Juni 30, mwaka huu, ambapo wizi hao hawakuvunja eneo lolote la chumba zilipokuwa zimehifadhiwa kwa muda, wakati ujenzi wa shule hiyo ukiwa katika hatua za mwisho.

Ukielezwa kuwa funguo za jengo hilo hazikuwa zimekabidhiwa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, na kwamba hadi walinzi waliokuwa wanailinda shule hiyo mpya, walikuwa chini ya kampuni iliyoijenga.

Awali, kompyuta hizo zilinunuliwa na wizara kisha zilikabidhiwa kwa uongozi wa muda wa shule hiyo tangu Machi 27, mwaka huu kisha Machi 30 zilitengenezewa fomu maaluma ya vifaa vilivyokuwamo.

Ofisa Mdhamini Wizara ya Elimu Pemba, Mohamed Nassor Salum, alisema alipokea kwa mshtuko taarifa ya wizi huo hasa kwa vile hakuna eneo la ukuta au mlango uliyovunjwa kabla ya wizi.

Alisema waligundua kuwa kompyuta hizo zilishaibwa baada ya watendaji wa wizara kufika ndani ya chumba zilimokuwa zimehifadhiwa wakiwa na walinzi wa kampuni kisha kupeleka taarifa hizo kituo cha Polisi Wete.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alisema taarifa hizo wameshazipokea, na wanawashikilia watu watatu kwa tuhuma za wizi huo.

## Mtuhumiwa wa kubaka mtoto asota rumande

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

ABDUL-NASSIR Salum Abass (20) mkaazi wa Kiuyu Kigongoni Wilaya ya Wete, anayetuhumiwa kumbaka mtoto wa miaka 17, anaendelea kusota rumande baada ya hakimu anayeshughulikia kesi hiyo kuwa nje ya mahakama kikazi.

Baada ya mtuhumiwa huyo kufika kizimbani akisubiri taratibu za mahakama, ndipo Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, Mohamed Said Mohamed, alipodai kuwa shauri hilo lipo kwa ajili ya kusikilizwa mashahidi, ingawa hakimu husika hayupo mahakamani.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo 'A' Hamad Suleiman, hakuwa na pingamizi juu la ombi la upande wa mashtaka na kusema shauri hilo litarudi tena mahakamani Julai 9, mwaka huu kwa ajili ya kusikilizwa.

"Mtuhumiwa hutakiwi kujibu chochote, kwani hakimu hayupo, hivyo shauri lako litasikilizwa mashahidi Julai 9, mwaka huu."

Awali ilidaiwa kuwa, mtuhumiwa alitenda kosa siku na tarehe isiyojulikana Agosti mwaka 2019 majira ya usiku katika maeneo ya Kiuyu Kigongoni Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa bila ya halali alimbaka msichana mwenye umri wa miaka 17.

## Utotoleshaji vifaranga samaki kuanza

**Mary Mshami na Magdalena Haule**

SERIKALI imesema mradi wa kutotolesha vifaranga vya samaki kwa ajili ya kukidhi soko nchini utaanza hivi karibuni ili kuchochea uchumi wa viwanda.

Mradi huo ni wa usimamizi wa uvuvi wa Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SwioFish), utakaotekelezwa Oktoba, mwaka huu.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu wa Mifugo na Uvuvi, Rashid Tamatamah, alipotembelea maonyesho ya Sabasaba.

"Mradi kama huu utasaidia kukuza sekta ya viwanda na uvuvi na kutoa elimu kwa wanafunzi ambao watapata fursa ya kujifunza kwa vitendo," alisema Tamatamah.

Alisema mchakato wa ujenzi wa mradi wa maabara ya vifaranga vya samaki Kunduchi umeanza na washirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na baada ya miezi mitatu ujenzi utaanza kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Kadhalika, alisema katika maonyesho ya Sabasaba ya mwaka huu, watatoa elimu kwa wavuvi ya kuvua samaki wa kuliwa.

# Halmashauri yalalamikiwa kwa kutimua w'biashara

**Na Stevie chindiye, TUNDURU**

WAFANYABIASHARA ndogo katika mabanda ya soko kuu, stendi kuu na stendi ya mabasi ya vijijini katika kata ya Nanjoka, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, wamelalamikia tamko la halmashauri linalowataka kuondoka katika vibanda wanavyofanyia biashara zao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwa masharti ya kutotaja majina yao, walisema malalamiko hayo yametokana na halmashauri kuchukua hatua hizo bila kuwahusisha wafanyabiashara hao ambao ndio waliojenga mabanda hayo kama hamasa ya kuendeleza eneo hilo.

Walisema awali eneo hilo halikuwa na kitu, lakini baada ya wananchi kukamilisha ujenzi huo, halmashauri ikaanza kuingilia kati na kuanza kuwatoza pango, huku kukiwa hakuna makubaliano yoyote kati yao.

Akizungumzia sakata hilo kwa niaba ya Mkurugenzi, Ofisa Mapato wa halmashauri hiyo, Obeth Mwakisole, alisema kodi inategemea ukubwa wa chumba, kulingana na mkataba wa upangishaji.

Alisema halmashauri inamtaka mmiliki wa kibanda awe na leseni ya biashara anayofanya kwenye chumba husika, lakini sehemu kubwa ya vibanda vilivyopo katika maeneo ya stendi, vinamilikiwa na watu ambao hawafanyi biashara.

Alisema kazi ya kubaini uwapo wa wafanyabiashara wanaopangisha vibanda hivyo ilifanywa na tume ambayo iliundwa na Mkuu wa Wilaya baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wanaoendesha shughuli zao katika mabanda hayo kudai kutozwa pango kubwa na watu wanaojiita wamiliki wa vibanda hivyo.

"Ni tabia ya watu wajanja kutaka kupata fedha kwa njia isiyokuwa halali, wanakiuka taratibu za ununuzi na kumekuwa na watu ambao hufikia hatua hata kuuziana mabanda hayo huku wakiwa hawakuyajenga wao," alisema Mwakisole.

Alisema lengo la halmashauri ni kumfanya mwananchi wa Tunduru anayefanya biashara katika maeneo hayo kupata faida kubwa ikiwa ni tofauti na wafanyabiashara ambao wamepanga katika mabanda yaliyopo nje ya vibanda vya halmashauri ambao wanatozwa pango kubwa na kuwafanya wapate faida ndogo.

"Hatutaki mgogoro na wananchi wetu bali tuwaite ili tuwaelimishe waache tabia ya kupangisha mabanda hayo, waende halmashauri wakae mezani ili warejeshewe gharama zao," alisema Mwakisole.

Hata hivyo, alisema baada ya uongozi wa halmashauri kukaa na kujadili walikubaliana kuwa kwa sasa hakuna mtu atakayefukuzwa katika vibanda hivyo.




Ofisa Mwendeshaji wa Benki ya TPB, Jennifer Liyumba (kushoto), akitoa maelezo kwa Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, alipotembelea banda la benki hiyo, katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa katika Uwanja vya Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiwanda cha nyaya chamridhisha Zungu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amekipongeza kiwanda cha kuzalisha nyaya za umeme cha Ok Plast kwa kufanya uzalishaji unaozingatia kanuni na taratibu za mazingira.

Aidha, amekiahidi kushughulikia changamoto ya uuzwaji wa taka za mabaki ya shaba nje ya nchi.

Akizungumza na wanahabari jana jijini Dar es Salaam baada ya kutembelea kiwanda hicho, Waziri Zungu alisema kiwanda hicho kinafanya uzalishaji mkubwa wa nyaya za umeme ambazo soko lake kubwa lipo nchini na kuahidi kushughulikia kero ambazo kiwanda hizo inakumbana nazo.

"Kiwanda kinafanya uzalishaji mzuri kwa kufuata kanuni na taratibu za mazingira, lakini wamekuwa na changamoto ya utunzaji wa taka baada ya kuyeyushwa kwa shaba ambayo kwa hapa nchini hazina soko. Nitaagiza timu ya wataalamu kuja kuangalia madhara yanayoweza kupatikana kwa kusafirishwa taka hizo nje ya nchi kabla ya kutoa kibali," alisema Zungu.

Alisema licha ya kushughulikia changamoto ya kiwanda hicho, amewataka wenye viwanda kuacha kuhujumu miundombinu ya umeme, maji na madaraja kwa lengo la kupata malighafi za kuzalishia nyaya za umeme.

Katika hatua nyingine amewataka wenye viwanda kuweka miundombinu rafiki katika kuhakikisha wanazuia kusambaa kwa hewa chafu ambayo imekuwa inazalishwa viwandani, hivyo kuleta athari kubwa kwa wakazi wa maeneo kuzunguka viwanda na pia kusababisha mabadiliko ya tabia nchi.

Ofisa Mazingira wa kiwanda hicho, Gilbert Grid, licha ya kupongeza ujio wa Waziri kiwandani hapo, alisema kiwanda chao kitaendelea kufanya uzalishaji kwa kufuata kanuni na taratibu zote za mazingira ili kujiepusha na migongano na taasisi za serikali ikiwamo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

"Kumekuwa na ufuatiliaji wa muda mrefu wa namna ya kusafirisha mabaki ya shaba (slime & slug) nje ya nchi ambako soko lipo, ujio wa waziri ambaye amejionea uzalishaji na uwapo wa mabaki hayo ni hatua muhimu kwa kiwanda kwa kuwa yanapobaki kiwandani tunakosa nafasi."

Naye Meneja wa NEMC Kanda ya Mashariki, Arnold Mapinduzi, aliwataka wenye viwanda wanaotumia malighafi za vyuma chakavu kufuata taratibu ikiwamo kununua malighafi hizo kutoka kwa wenye vibali vya ukusanyaji na usafirishaji.

## CRDB yasaidia shule, meza, viti

**Na Shaban Njia, MBOGWE**

HALMASHAURI ya Mbogwe wilayani Mbogwe mkoani Geita, imepokea viti na meza 153 kutoka benki ya CRDB kwa ajili ya shule za sekondari Masumbwe inayokabiliwa na uhaba wa viti.

Hali hiyo imesababisha baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo kusoma kwa zamu. Halmashauri hiyo inakabiliwa kuwa na uhaba wa viti na meza 1,942 katika shule za sekondari 16 zilizopo, huku zikiwa na jumla ya wanafunzi 8,975.

Akikabidhi vifaa hivyo, Meneja wa benki ya CRDB Kanda ya Magharibi, Said Pamui kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Math Mkupasi, alisema lengo la kutoa vifaa hivyo ni kutatua changamoto ya wanafunzi kusoma kwa awamu.

Akipokea vifaa hivyo DC Mkupasi alisema kuna uhitaji wa viti, meza na madawati katika shule za msingi na sekondari ni mkubwa na kuwaomba wadau na wazazi kushirikiana na serikali kuhakikisha tatizo hilo linapatiwa ufumbuzi.



## Ukimwona mtoto huyu toa taarifa

**Na Mwandishi Wetu**

MTOTO Fatuma Mwita (16) anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani kwao Makongo, jijini Dar es Salaama na kwenda kusikojulikana.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili, mama mdogo wa mtoto huyo, Gaudensia Mwita, alisema alitoweka Mei 9 mwaka huu, majira ya saa sita mchana na tayari taarifa zake zimefikishwa kituo cha polisi.

"Nilishatoa taarifa kituo cha polisi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kufungua jalada namba UD/RB/772/2020," alisema Gaudensia.

Gaudensia alisema, siku ya tukio, alichukua ndoo ya kutunzia taka wakadhani kwamba anapeleka jalalani kumbe ndani aliweka nguo zake na kutomea kusikojulikana.

"Ninawaomba wasamaria wema watakaomwona sehemu yoyote, watoe taarifa kituo cha polisi na pia watujulishe kwa namba 0655-626669 au 0719-311799 ili tuweze kumpata," alisema.

## Kasi ya mlungula makada CCM inavyoacha maswali

Ukurasa 12





Ukurasa 13

## Fursa wapigakura kutumia haki ya uhuru wa kujieleza



# Kasaka amekufa lakini ataishi

**Na Epson Luhwago**

ILIKUWA taarifa ya kushtua baada ya kupokea habari kuwa mwanasiasa mkongwe, mwenye misimamo thabiti na mwenye kusimamia na kuishi kile anachokiamini kuwa amefariki dunia.

"Naomba unielekeze nyumbani kwa Mzee Njelu Kasaka," ilikuwa simu ya Samson Mfalila, mhariri na mwandishi wa takriban miongo mitatu aliponipigia simu. Nilimuuliza kuna nini? Naye akajibu kuwa: "Amefariki dunia."

Hiyo ilikuwa Ijumaa Julai 4, mwaka huu, nilipopata habari hizo. Sikuamini taarifa hizo kwa sababu wiki moja iliyopita niliwasiliana naye akiwa nyumbani kwake Chunya akiendelea na shughuli zake.

Katika miaka ya karibuni, Kasaka amekuwa mtu wangu wa karibu, tukifanya kazi pamoja hasa katika mchakato mzima wa kuandaa na kuchapisha kitabu chake cha "Njelu Kasaka Maisha, Siasa na Hoja ya Tanganyika-G55" ambacho sasa ni moja ya vitabu gumzo nchini vilivyoandikwa na watu mashuhuri.



Njelu Kasaka 1942 - 2020

Mara kwa mara nilikuwa nawasiliana naye, tunakutana, kupata maoni na kufanya tathmini juu ya maendeleo ya mauzo ya kitabu hicho ambacho kwa sehemu kubwa kina mkono wangu hadi kukamilika kwake. Baada ya taarifa hizo kutoka kwa Mfalila, nilipompigia mtoto wake, Masache, alithibitisha kuwa taarifa hizo ni za kweli na kwamba alifariki dunia usiku wa kuamkia Ijumaa iliyopita katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, alikokuwa anapatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa Masache, Kasaka alifikishwa hospitalini hapo kutoka Chunya baada ya kuugua ghafla wiki moja iliyopita alipokuwa katika shughuli zake.

"Ni kweli baba amefariki (dunia) usiku wa kuamkia leo (jana) na hivi tunavyoongea msiba uko hapa nyumbani kwangu Mbeya mjini. Leo (jana) tunatarajia kusafirisha mwili wa mzee wetu kwenda nyumbani Chunya. Tunatarajia kumzika baba Jumapili (kesho)," alisema Masache huku akibainisha kwamba atapumzishwa katika nyumba yake ya milele kijijini Mtanila, takribani kilomita 100 kutoka Chunya mjini.

Taarifa hiyo ya Masache ilifuatiwa na taarifa nyingine ya mtoto wake, Chikulupi, ambaye katika mtandao wa kijamii kupitia ukurasa wake wa Facebook, alithibitisha hilo.

Hakika nilipatwa na mshtuko kwa sababu katika mazungumzo yetu akiwa Chunya, Kasaka alisema kuna mambo ya kuyazungumza na kutekeleza na kwamba tutaonana ndani ya wiki moja atakaporejea Dar es Salaam.

Maandiko matakatifu yanasema mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake za kuishi si nyingi. Pia maneno mengine yanasema siku za kuishi duniani ni miaka 70 na ikiwa tuna nguvu ni miaka 80.

Kwa hakika maneno hayo yamesadifu na maisha ya Mzee Kasaka ambaye ameishi duniani miaka 78 tangu alipozaliwa mwaka 1942 akiwa mtoto wa Mzee Mlugala Kasaka aliyekuwa Chifu wa kabila la Wakimbu na mama yake Zena.

Pamoja na kwamba hakuna mwanadamu ajuaye mwisho wa kuishi duniani (kifo chake), huenda Kasaka aliongozwa na Mungu hadi akaweka historia na mambo aliyoyafanya maishani mwaka kupitia kitabu chake.

"Nilikuwa na mawazo ya kuandika vitabu vingi hasa vya kitaaluma kutokana na elimu yangu lakini nimeona ni vyema niandike historia yangu na mambo niliyoyafanya katika maisha yangu ya kawaida, utumishi na siasa.

"Baadhi ya mambo haya huwezi kuyakuta mahali popote. Hata hii hoja ya Tanganyika na yaliyojiri katika mchakato mzima hakuna mwenye kumbukumbu yake. Hata wakati nawasilisha hoja bungeni, mitambo ya Hansard (kumbukumbu rasmi za Bunge) ilizimwa," alisema Kasaka katika moja ya vikao vya maandalizi ya kitabu chake.

Ikiwa mwaka mmoja na nusu tangu kitabu chake kitoke na kuingia sokoni, maisha yake yamefikia tamati. Hiyo ndiyo picha inayoonekana kuwa alitambua kuwa ipo siku atazimika lakini ni vyema aache alama ambayo itamfanya akumbukwe muda mrefu.

Katika kuthibitisha hilo, alidokeza kuwa watu wengi maarufu wanakufa bila kuweka kumbukumbu zozote juu ya mambo waliyofanya na matokeo yake wanasahaulika haraka.

"Nimeona niweke hili jambo ili vizazi vya sasa na vijavyo vikisoma vitapata elimu kuhusu mambo yaliyofanyika kwenye siasa za Tanzania," alisema.

**ATAKUMBUKWA**

Kasaka ametangulia mbele za haki lakini historia yake haitafutika. Kupitia kitabu chake, kizazi kwa kizazi kitajifunza na kumfahamu kwa kina kuhusu mambo mengi aliyoyafanya katika siasa, utumishi wake na maisha yake ya kawaida.

Jambo la kwanza ambalo atakumbukwa ni ujasiri wake wa kusimamia kile alichokianzisha huku akiamini kuwa ni cha kweli na hawezi kusimamishwa wala kukatishwa tama na mtu yeyote.

Hilo linajionyesha katika hoja yake akiongoza kundi la wabunge 55, maarufu kama G-55 ambalo lilikuwa likidai kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika baada ya Zanzibar kukiuka Katiba ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo kujiunga na Jumuiya ya Kiislam (OIC).

Miongoni mwa wabunge hao walikuwa William Mpiluka (Mufindi), Paschal Mabiti (Mwanza Mjini), Patrick Qorro (Karatu), Arcado Ntagzwa (Kibondo), Mbwete Hombee (Mbeya Vijijini), Christian Fundisha (Tabora Kusini), Guntram Itatiro (Ulanga), Sebastian Kinyondo (Bukoba Vijijini), Jenerali Ulimwengu (Taifa) na Tabitha Siwale (Taifa).

Kasaka na wenzake, pamoja na kuitwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na kuwataka kuachana na mpango huo, walimkatalia na kumwambia hawawezi kurudi nyuma. Sambamba na hilo, akiwa meneja wa CRDB Iringa, alimfukuza mfanyakazi aliyekuwa amefanya makosa na viongozi wa makao makuu walipomtaka afute uamuzi wake, aliwagomea kwa kuwa aliamini kuwa alikuwa sahihi katika kuchukua uamuzi huo.

Kitu kingine ambacho kitamfanya akumbukwe ni ufuatiliaji wa mambo alipokuwa mbunge, naibu waziri na mkuu wa mkoa. Akiwa mbunge, kwa mfano, alifuatilia suala la umeme hatua kwa hatua kwa kuwafuta wahusika wakiwamo makatibu wakuu wa wizara na hatimaye kufanikisha azma yake. Hivi ndivyo alivyokuwa akifanya katika maisha yake yote kwani alikuwa akihakikisha makubaliano yoyote lazima yatekelezwe kwa wakati walioafikiana.

**HISTORIA YAKE**

Njelu Kasaka alizaliwa mwaka 1942 Chunya mkoani Mbeya na alianza elimu ya 'Bush' mwaka 1955 na 1956 kabla ya kujiunga na Shule ya Msingi Kipambawe hadi mwaka 1960 alipomaliza darasa la nne.

Alifaulu vizuri kwa kushika namba moja kati ya watoto 45 na kujiunga na Shule ya Kati (Middle School) Chunya alikosoma hadi darasa la nane. Baada ya hapo alijiunga na Shule ya Sekondari Tosamaganga ambako alisoma kidato cha kwanza na cha pili lakini alikatisha masomo kidato cha tatu kutokana na matatizo ya kiafya. Alihamia Sangu alikosoma kidato cha tatu na cha nne.

Mwaka 1968 alifanya mtihani wa kidato cha nne na kufaulu kisha kujiunga na Shule ya Sekondari Mkwawa, Iringa, kwa masomo ya kidato cha tano na cha sita. Baada ya hapo alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1971 na kuhitimu shahada ya kwanza ya Uchumi.

Baada ya hapo aliajiriwa na Benki ya Maendeleo Vijijini (TRDB) ambayo baadaye ilibadilishwa jina na kuitwa Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini. Mwaka 1978 alijiunga na Chuo Kikuu cha Kentucky, Marekani kwa masomo ya shahada ya uzamili ya Uchumi katika Kilimo na kuhitimu mwaka 1980. Pia alikuwa na diploma ya uchumi kutoka Taasisi ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Colorado, Marekani.

# Kasi ya mlungula makada CCM inavyoacha maswali




Wanaccm wakiwa kwenye harakati za kampeni.**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Sabato Kasika**

MWEZI huu ni wa muhimu kwa CCM kwa kuwa ndiyo msimu mchakato wa uchaguzi mkuu unapoanzia kupata wagombea wa ubunge, urais na madiwani.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, anawaambia wanahabari kuwa mchakato huo unalenga kupata makada sahihi wa kupeperusha bendera ya CCM kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Lakini, pia anasema CCM haitaki makada wavurugaji na kwamba chama hakitawavumilia watakaofanya vurugu na kuwa kimbelembele na kwamba kimeweka mitego kuwanasa.

Anasema, CCM imeiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kuwanasa wafanya fujo na kwamba majina yao yatakatwa. Pamoja na maonyo hayo, inaonekana baadhi ya makada wameweka pamba masikioni wakifanya mambo yanayowatumbukiza mikononi mwa dola.

Hii inatokana na ukweli kwamba tangu chama kutangaza kufungua dirisha la kuchukua fomu za kuwania nafasi za kugombea, kumekuwapo na taarifa za kukamatwa kwa baadhi ya makada, kwa tuhuma za rushwa.

**KWANINI RUSHWA?**

Tangu CCM itangaze mkakati wa kushirikisha Takukuru ili kukomesha rushwa ndani ya chama hicho, kumekuwapo na taarifa za kukamatwa kwa baadhi ya makada kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Kwa mfano, taarifa iliyotolewa Juni mosi mwaka huu na Takukuru Mkoa wa Kinondoni, inatangaza kuwashikilia viongozi watano wa CCM, kwa tuhuma za rushwa na kuanza kampeni mapema kabla ya muda. Juni 3 mwaka huu, Takukuru Mkoa wa Mtwara, anawaeleza wanahabari kuwa wana CCM 18 wakiwamo viongozi wa Kata ya Mlingula, wamekamatwa.

Wanatuhumiwa kufanya kikao kisicho halali ili kushawishi uungwaji mkono kwa mgombea aliyetia nia kugombea ubunge wa jimbo la Ndanda lililopo wilaya ya Masasi mkoani humo. Aidha, mwishoni mwa mwezi uliopita, Takukuru mkoa wa Arusha, alitangaza kuwashikilia watu tisa wakiwamo viongozi wa Jumuiya ya Wazazi kwa makosa mbalimbali ya rushwa.

> “Wagombea wasio na kitu mfukoni, rushwa iliwatenga na mbaya zaidi ni kwamba hakukuwa na dhamira ya dhati ya kuiondoa, lakini sasa ni wazi ipo azma ya kuikomesha ili kupata viongozi kihalali.




Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbung'o, taasisi hiyo imenasa makada kadhaa rushwa za uchaguzi.

Mkoani Shinyanga, taasisi hiyo ilimnasa mfanyabiashara (jina linahifadhiwa) akiwa na doti 600 za vitenge vyenye nembo ya CCM vilivyokuwa vikidaiwa kutumika kushawishi wapigakura kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020.

Mkoani Lindi mkono mrefu wa Takukuru umetua kwa mtiania wa ubunge jimbo la Mtama mkoani humo (CCM) kwa tuhuma za rushwa.

Kutokana na kuwapo kwa tuhuma za kunaswa kwa baadhi ya makada wa CCM kwa rushwa, wachambuzi wa masuala ya siasa wametoa maoni tofauti wapozungumza na gazeti hili kuhusu tuhuma hizo.

Mchambuzi Deus Kibamba, anasema, mfumo wa uchaguzi uliopo ndiyo ambao unaendekeza kuwapo kwa rushwa, hivyo ni vigumu kuimaliza hadi hapo mfumo huo utakapobadilishwa.

“Mfumo uliopo katika uchaguzi wetu ni kuchagua mtu, hivyo ni rahisi mgombea kuhonga wapigakura ili waweze kumchangua, ndiyo maana nikasema mfumo huo unaendekeza rushwa,” anasema Kibamba.

Anasema, kama Tanzania inataka iachane na rushwa katika uchaguzi, iige mfumo wa Afrika Kusini, ambao ni wa kuchagua chama badala ya mtu ili iwe rahisi kubabiliana na tatizo hilo.

“Kule wanapigia kura chama, ambacho kinapata kura nyingi ndicho kinachoteua rais na hata kwa wabunge, kikipata asilimia 82 ya kura ni wazi wagombea 60 hadi 80 wa ubunge, wote watapata nafasi,” anasema.

Anasema, mfumo umesaidia kumaliza tatizo la rushwa katika uchaguzi nchini humo, hivyo wakati sasa wa Tanzania kuiiga ili kuondokana na kamatakamata ya watia nia inayoendelea kila kona ya nchi.

“Kwa kawaida anayepewa rushwa ni mtu, hivyo kwa mfumo wa kupigia kura chama itakuwa ni dawa ya kukomesha tatizo hilo kwa sababu chama hakihongwi wala hakipokei rushwa,” anasema Kibamba.

Anasema, kuendelea kwa mfumo wa sasa hakutasaidia kukomesha mtindo huo, kwa madai kwamba, wanasiasa wengi wanatafuta kula, hivyo wanafanya kila njia ikiwamo kutoa rushwa ili kutimiza malengo yao.

**KUZOEA KUNYONGA**

Wakati Kibamba akisema hayo, mchambuzi mwingine, Abdulkarim Atiki, anasema, wanaonaswa kwa tuhuma za rushwa ni wale ambao wamezoea vya kunyonga, hivyo vya kuchinja hawaviwezi.

Aidha, anasema, hao ndiyo ambao bado wanaamini CCM ni ile ile bila kutambua kuwa imebadilika, chini mwenyekiti wake Dk, John Magufuli, na imekuwa mpya isiyokumbatia vitendo vyote viovu.

“Ni muhimu wanachama wakasoma ishara za nyakati na kuachana na makandokando yote, kwani CCM ya sasa inasimamia misingi ya haki kwa wote bila kujali ukabila, udini na urafiki,” anasema Atiki.

Atiki anasema, wale wasiozingatia hilo wataendelea kukamatwa hadi nidhamu irudi kwenye chama, kwa vile rushwa ilikuwa ni tatizo kubwa ndani ya chama na kusababisha wanachama wengine kukosa haki.

“Sina budi kuwapongeza viongozi wa CCM wa awamu hii kwa kuiona rushwa na kuivalia njuga kwani ilichangia kupitisha makada wasio na sifa katika chaguzi mbalimbali,” anasema.

Mchambuzi huyo anasema, rushwa ilianza kulelewa muda mrefu ikiwa inabadilishwa majina kuanzia takrima, bakshishi, chai, kifuta jasho na kuwa kikwazo kwa wagombea wenye sifa.

“Wagombea wasio na kitu mfukoni, rushwa iliwatenga na mbaya zaidi ni kwamba hakukuwa na dhamira ya dhati ya kuiondoa, lakini sasa ni wazi ipo azma ya kuikomesha ili kupata viongozi kihalali,” anasema.

Anaeleza kuwa ilikuwa ni mazoea kwa makada wa CCM kwenda kwa wapigakura na kuwapa rushwa, na kwamba sasa wasome ishara za nyakati ili wasiingie katika mtego, ambao mwisho wake wataumbuka na kujihaharibia matarajio yao ya baadaye.

“Chama kinasema, rushwa marufuku kwa wagombea, kinataka kupata viongozi waadilifu na kuwapo kwa usawa wa ushindani wakati wa mchakato, hivyo wahusika wasome ishara za nyakati,” anasema.

**ISIWE KUHARIBIANA?**

Kwa upande wake kada wa CCM Thomas Ngawaiya, anasema, ni vyema wanaokamatwa wawe wamethibitika kuhusika na utoaji rushwa na pia wapokeaji rushwa nao wanaswe kwa vile wote kosa lao ni moja.

“Ninasema ithibitike, kwa sababu kukamata kabla ya kuthibitisha tuhuma, kunaweza kuwaondolea watuhumiwa hadhi katika jamii kwa ajili ya malengo yao ya baadaye kwenye siasa,” anasema Ngawaiya.

Anasema, hapingani na kazi ya Takukuru, bali anaamini kwenye siasa kuna mambo mengi yakiwamo ya kuharibiana, lakini pia anaamini kuwa hadi taasisi hiyo kufikia kukamata watuhumiwa itakuwa imejiridhisha pasipo shaka.

Labda nitoe angalizo kwa watia nia kwamba wawe makini, watafute nafasi kihalali, kwa sababu wanatafuta kutumia wananchi, basi watafute uongozi kwa njia safi bila kukumbwa na tuhuma za rushwa,” anasema.

Ngawaiya anasema, wakati huu ambao chama kimeruhusu watia nia kujipitia kwa wananchi, ni vyema wakakikisha wanaepuka kujihusisha kwa namna na utoaji au upokeaji wa rushwa.

# Fursa wapigakura kutumia haki ya uhuru wa kujieleza

**Na Mwandishi Wetu**

OKTOBA, mwaka huu taifa linatarajia kufanya uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na raisi. Eneo mojawapo la msingi ni wapigakura kuamua watu wanaotaka kuwapa dhamana ya kuwawakilisha ili kuwasemea mambo yao iwe bungeni, kwenye halmashauri na ngazi zote za kufanya uamuzi. Kwa hiyo kinachotegemewa ni kutoa ya moyoni. Kueleza kinachowakwaza. Kuzungumza upungufu , changamoto na njia wanayodhani inafaa katika kuwawakilisha na kuwaletea maendeleo ili waondokane na umaskini.

Hili linafanyika kwa kutumia haki ya kujieleza na kutoa maoni. Ili kufahamu zaidi, Nipashe inazungumza na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma, Sabatho Nyamsenda kuhusu umuhimu wa silaha hii wakati huu wa uchaguzi mkuu. Anaanza kuelezea haki hiyo kikatiba.

Uhuru wa kujieleza ni haki ambayo imelindwa kikatiba. Ukisoma ibara ya 18(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatamka wazi kuwa "kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake na kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana zozote kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi, na pia uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa kati." Kifungu cha 2 cha ibara hiyo kinaweka haki ya kupata habari kama haki ya msingi kwa kila mwananchi.

**SWALI:Uhuru wa kujieleza una umuhimu gani wakati wa uchaguzi mkuu?**

**JIBU:** Haki ya uhuru wa kujieleza ni ya muhimu na ya msingi, hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu, kwa sababu wananchi wanapaswa kuitumia kufuatilia, kuhoji na kuamua juu ya watu wanaotakiwa kupewa dhamana ya kuwawakilisha katika ngazi mbalimbali za maamuzi.

Hivyo, haki ya wananchi kutoa maoni yao bila hofu ya kuadhibiwa na dola na kushiriki katika mikutano ya kisiasa ni vema ikazingatiwa. Bila kuwepo kwa uhuru wa kujieleza basi uchaguzi hauwezi kuwa kamili, na wala hauwezi kutambuliwa kuwa wa huru na wa haki.

Katika nchi kama Tanzania mapambano ya kudai haki ya uhuru wa kujieleza yanaendelea. Mapambano hayo huchukua sura tofauti kulingana na nafasi ya kitabaka ya wapambanaji. Watu wa tabaka la juu na kati hutazama uhuru wa kujieleza kwa miwani finyu ya kisheria pekee.

Kwa hiyo, usawa na haki hutazamwa kama dhana za kisheria, kwamba kila mtu yupo sawa mbele ya sheria. Lakini kiuhalisia hali ni tofauti. Kwa mfano mmiliki wa kampuni ya mabasi na mwajiriwa wake, ambaye ni dereva, hawawezi kuwa sawa. Mmiliki ana nguvu kuliko mfanyakazi na mwajiri ana mamlaka ya kumfanyisha kazi mwajiriwa kama punda huku akimpunja mshahara. Lakini watu wengi wa tabaka la juu hawapendi mambo haya ya unyonyaji wa kitabaka yazungumzwe. Kwao, uhuru wa kujieleza huwa ni haki tu ya kutoa maoni pekee lakini si kugusia madhila wanayoyapata watu wa tabaka la chini.



Wanawake, kundi kubwa la wapigakura wenye stahiki muhimu katika kupaza sauti zao. **PICHA: MTANDAO**

> Halikadhalika, kwa mijini wamachinga ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakitimuliwa katikati ya majiji na miji yetu, wamekuwa wakipambana kuendelea kubaki katikati ya jiji.

Kwa hiyo, haki ya uhuru wa kujieleza inapotazamwa kwa miwani ya tabaka juu na kati huwa inapoteza muktadha wa kijamii. Hubaki kuwa dhana ya kisheria peke yake ya kuelezea mapambano ya wananchi dhidi ya dola. Demokrasia, ambayo dhana ya kujieleza ni kiashiria muhimu, nayo hubakia kuwa ulingo wa wanasiasa kugombania vyeo na ujenzi wa taasisi zenye kulinda minyukano hiyo ya wanasiasa. Sasa, japokuwa kila mwanasiasa husema kwamba anagombania uongozi, uwe ubunge au udiwani, kwa ajili ya kupigania maslahi ya wananchi, kusema kweli wananchi hao huwa ni ngazi tu ya kumfikisha katika pepo ya hadhi ya juu, maisha ya raha, na utajiri wa fedha.

**SWALI: Watu wengi wanaona kuwa umuhimu wa wananchi kutumia haki ya kujieleza iko mijini zaidi na vijijini hawajaweza kutumia haki ya kujieleza, unalizungumziaje hilo?**

**JIBU:** Haki ya kujieleza inajumuisha haki ya tabaka la wavujajasho kupambana dhidi ya tabaka la washika dola na tabaka la watu wenye nguvu ya mtaji. Ukienda vijijini, utashangaa kukuta kuna kampuni inayojiita mwekezaji imetwaa ardhi ya kijiji kizima, na wananchi wanabomolewa makazi yao na kuchomewa mashamba yao.

Wengine huswekwa ndani na hata kubambikiwa kesi na kuishia gerezani. Wazalishaji hao vijijini huitumia haki hiyo hiyo ya uhuru wa kujieleza kama msingi wa madai yao ya kumiliki njia kuu za kiuchumi na kufaidika na jasho lao, pamoja na kudhibiti na kunufaika na rasilimali za taifa.

Halikadhalika, kwa mijini wamachinga ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakitimuliwa katikati ya majiji na miji yetu, wamekuwa wakipambana kuendelea kubaki katikati ya jiji.

Kwa hiyo, ikitazamwa kwa miwani ya wanyonge haki ya uhuru wa kujieleza huwa ni sehemu ya mapambano ya haki-jamii (social justice). Haitenganishwi na mapambano ya kuondoa unyonyaji, ukandamizaji na uporaji wa rasilimali unaofanywa na tabaka la 'walalaheri' walio na nyadhifa katika dola au nguvu za fedha.

Ni muhimu basi, tunapoizungumzia haki hii twende mbali zaidi na kuitazama kwa miwani ya tabaka la wanyonge, wavujajasho ambao ndio wapiga kura wakuu.

**SWALI: Unadhani ni kwanini wanawake ambao ni wapigakura wakuu wanatakiwa kuutumia uhuru huu wa kutoa maoni wakati huu?**

**JIBU:** Ni kweli kuwa, kwa idadi, wanawake ndiyo wengi, na ndio mhimili wa uchumi wa nchi hii kisiasa na kiuchumi. Wanawake ni mhimili kiuchumi, kwa sababu ndio wazalishaji wakuu. Kundi hilo ndilo linalozalisha mashambani, ndiyo waliojaa masokoni wakisambaza bidhaa na hawa waliobeba jukumu kubwa la kutunza familia. Kisiasa, kinamama ndiyo wapiga kura wakuu, kwa sababu hiyo vyama vya siasa hufanya kila namna kupata kuungwa mkono na wanawake. Kwa hiyo, wanawake ndio uti wa mgongo wa uchumi na siasa yetu.

Hivyo, wanawake wanapaswa kuutumia uhuru wa kutoa maoni kuelezea madhila yanayowakumba nayo kutokana na mfumo wa kiuchumi uliojikita katika uporaji wa rasilimali na haki zao. Aidha, wazungumzie mfumo wa kisiasa uliojikita katika hadaa na mfumo dume ambao umetamalaki katika nchi nyingi za Kiafrika.

Mfumo huo ndiyo unaowafanya wanawake watembee kilometa nyingi kutafuta maji. Kadhalika, ndio unaosababisha uporaji wa ardhi vijijini, kuendeleza mila potofu, kuumiza wanawake wanaokabiliwa na mimba na ndoa za utotoni.

Pia ndiyo unaosababisha wafilisiwe mali zao kwa kuwahadaa wachukue mikopo yenye riba kubwa isiyolipika, na ndicho chanzo cha kuwalazimisha kutoa rushwa ya ngono kwenye uchaguzi wanapotaka kugombea nafasi za uongozi na pia japo ni wapiga kura wakubwa kuwalaghai kwa khanga na vitenge wakati wa uchaguzi kisha kuwatelekeza baada ya mgombea kuchaguliwa.

Wanawake wautumie uhuru wa kujieleza kuyaibua madhila yote yanayowakumba, na wawapime wagombea kutokana na sera wanazozinadi katika kuyaondoa mateso hayo. La muhimu zaidi, wanawake wavujajasho washikamane na kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi ili wachague viongozi wanawake wavujajasho wenzao watakaokwenda kusimamia ajenda ya ukombozi wa wanawake na wavujajasho wa nchi hii.

Hata baada ya uchaguzi, waitumie haki hiyo ya uhuru wa maoni katika kuwawajibisha wanasiasa na kuendeleza mapambano ya ujenzi wa mfumo wa kiuchumi unaolinda maslahi ya walio wengi na mfumo wa kisiasa unaodhibitiwa na kutimiza matakwa ya walio wengi na kuhakikisha usawa wa kijinsia.

**SWALI: Japo haki ya kutoa maoni iko ibara ya 18 ya Katiba, Watanzania wengi hawaifahamu. Je, taifa linahitaji kuwa na elimu ya uraia wakati huu wa uchaguzi mkuu kuhamasisha kutumia haki hiyo? Ni nani atakayewapa elimu hiyo, ni NEC au NGOs?**

**JIBU:** Inawezekana kuwa Watanzania walio wengi hawafahamu ibara ya 18 ya katiba ya nchi yao inasemaje, lakini hii haimaanishi kuwa hawaitumii haki hiyo katika mapambano yao. Mapambano ya kila siku ya wavujajasho kudai haki za ardhi, haki za kupata maji safi na salama, huduma za afya, kupinga manyanyaso au ukandamizaji wa wawekezaji na badhi ya viongozi yanadhihirisha namna wanavyouweka uhuru wa kujieleza katika vitendo, japokuwa hawanukuu katiba.

Lakini kila mwananchi anayo haki ya kufahamu sheria mama ya nchi inampatia haki, wajibu na mamlaka yapi. Hivyo ni muhimu zifanyike jitihada za kuhakikisha kuwa katiba inasambazwa kwa wananchi, na mijadala inaibuliwa kutokana na katiba hiyo. Wajibu huu ni wa vyombo vyote iwe ni vyombo vya habari, vyuo vikuu, asasi zisizokuwa za kiserikali, na vyombo vya kusimamia uchaguzi kama Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na hata vyama vya siasa. Jambo moja ambalo taasisi hizi zitapaswa kuzingatia pale zinapozungumza na wananchi ni kuchana na kasumba ya tabaka la juu ya kuwachukulia wananchi walio wengi kama kielelezo cha ujinga na kutokuwa na elimu.

Hiyo ni dhana potofu iliyojengwa katika misingi ya dharau dhidi ya uzoefu na maarifa ya walio wengi. Uzoefu katika uzalishaji na mapambano ya kudai haki ni elimu tosha ambayo wananchi walio wengi wanaipata katika mazingira yao. Kwa hiyo, kinachohitajika ni kutumia uzoefu huo kama msingi wa kuibua mijadala juu ya masuala ya msingi ya kitaifa, zikiwemo haki za kikatiba.



Rais John Magufuli, katika tukio la kuwaapisha wateule wake. **PICHA: MTANDAO**

# Magufuli na dhana ya viongozi kuridhika

**Na Mashaka Mgeta,** TABORA

KWA muda mrefu sasa, Rais John Magufuli, amewakumbusha watumishi wa umma aliowateuwa kwenye nyadhifa mbalimbali za kiongozi, kuridhika na kuwa wabunifu zaidi katika kuzikabili changamoto zilizopo kwenye jamii.

Rais Magufuli anasema kero zilizopo kwenye jamii ni nyingi na zinahitaji ubunifu na ushiriki wa hali na mali wa wateuliwa wake kuzitatua.

Katika hali inayoonyesha kutoridhishwa kwake, Rais anawashangaa wateuliwa wanaoshindwa kukamilisha malengo ya uteuzi wao, badala yale wanajawa na shauku, kiu na tamaa ya kutwaa nyadhifa nyingine hasa ubunge.

Awali, Rais Magufuli alishaweka bayana kwamba ni vigumu kwa viongozi wa aina hiyo hasa wanaotaka kuwania ubunge kupitia CCM anayoiongoza kupitishwa ili watimize azma hiyo.

Na katika kusisitiza nia hiyo, Rais Magufuli anatoa mfano wa viongozi wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama Mkuu wa Majeshi (CDF) Mabeyo na Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), kuwa atawashangaa kwenda kuwania ubunge ili wateuliwe kuwa mawaziri.

### TAFSIRI KINADHARIA

Zipo nadharia nyingi zinazoweza kuhusishwa na kauli hiyo ya Rais Magufuli, miongoni mwa hizo ni kuonyesha uzito wa namna anavyokerwa na tamaa ya madaraka kwa baadhi ya wateuliwa wake.

Paschal Shija, mwanataaluma ya sayansi ya siasa na mkazi wa Urambo mkoani Tabora anasema, hatua ya Rais kutumia nyadhifa za juu katika taasisi nyeti nchini, ni ishara ya kuonyesha ugumu uliopo kwa wateuliwa watakaokiuka tamko lake.

"Tafsiri yangu kwa kauli ya Rais Magufuli kuwahusisha IGP na CDF kama mfano wa kukemea wateuliwa wenye uchu wa madaraka, ni ishara ya kuonyesha ukubwa wa namna anavyokerwa na vitendo hivyo, lakini zaidi akitaka kuona jambo la msingi ni kutatua kero za wananchi na siyo kukimbilia madaraka na uongozi," anasema Shija.

> Unapoutazama uongozi wa Magufuli si ule wenye kutaka kujikweza, unaowalenga watu katika kupata suluhu ya matatizo yao hasa umasikini.

Kiongozi mmoja wa halmashauri ya wilaya ya Urambo anayeomba jina lake lisitajwe gazetini, anaunga mkono agizo la Rais Magufuli na kusema kuwa zipo kero nyingi kwenye jamii zinazohitaji nguvu kubwa ya utaalamu, ujuzi na usimamizi bora ili kutimiza malengo ya serikali.

"Ni vigumu sana kwa mtu mwadilifu na mwenye nia ya kuleta mabadiliko kwa maendeleo na ustawi wa watu kuacha nafasi aliyoteuliwa kama wakuu wa wilaya, wakurugenzi watendaji wa maendeleo katika halmashauri, makatibu tawala na wengineo na kutaka kuwa wabunge," anasema mtumishi huyo.

Anafafanua kuwa wananchi wengi katika ngazi za msingi wanaohudumiwa na watumishi katika serikali za mitaa na tawala za mikoa, wanakabiliwa na kero nyingi ambazo, kwa kiongozi na mtumishi mwadilifu, hawezi kufikiria kujitafutia manufaa yake binafsi.

"Ukimuona mtu anaacha kuwatumikia wananchi katika ngazi za msingi, badala yake akakimbilia nyadhifa za juu kama ubunge, huyo hafai. Huwezi ukawaacha wananchi katika matatizo yao ukaenda kutafuta uheshimiwa kwa kigezo cha kukerwa na kero ulizozikimbia, haiwezekani..." anasema.

### KUFIKIA MAFANIKIO

Furaha Dimitrious, anayeongoza taasisi ya Afya na Ustawi wa Jamii (Comheswa) anasema ipo haja kwa Watanzania kujikita katika matumizi ya rasilimali zilizopo, na kutafuta nyingine za ziada ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

Anasema ingawa nia ya ustawi wa jamii inapaswa kuanzia kwenye ngazi ya familia, lakini tamaa na uchu usiokuwa na malengo ya kutatua kero za jamii, haviwezi kuleta mageuzi, mabadiliko na maendeleo, hivyo anaungana na tamko la Rais Magufuli.

"Unapofanya kazi kwenye jamii na kufikia malengo yaliyousudiwa ni moja ya mafanikio makubwa yanayokufungulia njia ya kupita kwenda juu, ukilazimisha kupanda juu wakati kidogo ulichopewa kimekushinda, haiwezekani ukawa bora, ni tamaa tu na si nia thabiti ya kuleta mabadiliko na maendeleo" anasema.

Pamoja na Rais Magufuli kukemea wateule wenye uchu wa kwenda kuwania ubunge, wiki hii amesema hawezi kuzuia kuwapa ruhusa na kuwaalika wenye nia hiyo kumuandikia barua, naye atawaruhusu.

Ni mwito unaotoa mwanya wa kutimiza matakwa ya wateuliwa wenye nia za kuwania ubunge, lakini ukizungukwa na ugumu wa kupitishwa hasa kupitia vikao vya CCM ambavyo Rais Magufuli ni Mwenyekiti wake.

"Haiwezi kuwa rahisi kwa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa CCM, akemee kitendo cha kuacha wadhifa wa utumishi aliokuteua halafu apitishe jina lako kuwa mgombea ubunge, hiyo ni ngumu sana ninavyoona," anasema Francis Mgaya, kijana mwendesha pikipiki maarufu kama bodaboda wa mjini Tabora.

Wateuliwa wa nafasi mbalimbali za utumishi serikalini, wameripotiwa kutia nia ya kutaka kuwania ubunge, wengine wakianza mapema baada ya uteuzi wao, hali iliyozua migogoro kwa baadhi ya maeneo ya utawala nchini.

Hata hivyo, vyama kadhaa ikiwemo CCM vipo katika hatua tofauti za mchakato wa kuwapata wagombea urais, ubunge, ujumbe wa baraza la wawakilishi Zanzibar na udiwani ambapo majina yatakapotangazwa rasmi, watajulikana miongoni mwa wateuliwa, watakaopitishwa kuwania nafasi hizo.

Adelina Zakayo, mwanafunzi wa sayansi ya jamii katika Chuo cha Mtakatifu Augustine Tqanzania (SAUT), anasema aina ya uongozi unaoonyeshwa na Rais Magufuli unapaswa kuwa mfano na kioo kwa watumishi hasa wanaoteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi.

"Unapoutazama uongozi wa Magufuli si ule wenye kutaka kujikweza, unaowalenga watu katika kupata suluhu ya matatizo yao hasa umasikini," anasema mwanafunzi huyo.

Kwa mujibu wa Adelina, nchi inapokuwa na Rais mwenye mamlaka makubwa, kujiepusha na mambo yanayochangia matumizi makubwa ya rasilimali za nchi, inakuwa ni kielelezo cha nia njema ya kufikia maendeleo pasipo kuweka kando changamoto zilizopo.

"Rais Magufuli hayupo kwenye matumizi makubwa ya fedha, kwa mfano tangu aingie madarakani hajasafiri nje ya bara la Afrika, na hata humu Afrika amekwenda nchi chache, unaweza kuona ni kwa namna gani akili yake imewalenga Watanzania na kero zao," anasema.

Adelina anaona kwamba viongozi wa aina ya Rais Magufuli wapo wachache kwa vile safari za ughaibuni ni miongoni mwa vyanzo vinavyotoa mwanya kwa watawala wengi kuzitumia fursa zinazochochea matumizi makubwa ya rasilimali za nchi zao.

Ni dhahiri kwamba nia ya Rais Magufuli kuwataka wateuliwa wake kuridhika na nafasi walizonazo ni njema, na wanaokiuka agizo hizo wanaonyesha kutojua nia ya kiongozi huyo mkuu wa nchi kuwateua.

***Maoni: 0754 691 540, mgeta2000@yahoo.com.***





# Waziri aagiza kukamatwa madaktari vishoka wa mifugo

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ameagiza kukamatwa kwa madaktari wa mifugo vishoka ambao hawana ujuzi wa kutoa huduma za afya ya mifugo.

Aidha, ametoa maagizo 25 kwa bodi tatu zinazohusika mifugo na uvuvi huku akisema wataoshindwa kutekeleza uteuzi wao utatenguliwa wakati wowote.

Mpina alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na wajumbe wa kuzindua bodi ya Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA), Baraza la Vetenari Tanzania (VCT) na Bodi ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU).

Aliagiza bodi hizo kuhakikisha zinasimamia vizuri maadili ya madaktari kwa kukamata vishoka wote ambao wanatoa huduma za afya za mifugo nchini huku wakijua kuwa hawana ujuzi huo.

"Kuanzia leo natoa agizo na katazo kwa watu wasio na sifa yaani vishoka ya kutoa huduma za afya ya wanyama ni marufuku kabisa katika nchi yetu, tena tukikutana na mtu anaitwa kishoka nisiendelee kulisikia," alisema.

Alisema katika marekebisho ya sheria ambayo yanafanyika yanatakiwa yaendane na hasara ambayo kishoka anatakiwa kumlipa mfugaji kutokana na hasara aliyoisababisha kwa kutoa dawa au tiba isiyostahili.

"Adhabu ya kulipa faini haitoshi kishoka anatakiwa amlipe fidia mfugaji wetu aliyepata hasara ya mifugo yake kufa kwa sababu amedanganywa na kishoka huyo," alisema.

Alibainisha kuwa mtu ambaye hajasomea fani husika ataweza kutoa dawa kwa kuzidisha dozi au na kusababisha vifo vya mifugo.

Alisema mabaraza hayo yahakikishe yanaboresha huduma za afya za wanyama kwa kushirikiana na sekta binafsi wahakikishe wafugaji wanapata huduma sahihi.

Pia, aliyaagiza mabaraza hayo yote kuhakikisha wanasimamia ukusanyaji wa mapato na maduhuli yote ya serikali angalu kufikia makusanyo ya Sh. bilioni moja kwa mwaka tofauti na yaliyokuwapo ya Sh. milioni 251 kwa sasa.

Aidha, aliagiza mabaraza la vetenari kuwafuta kwenye orodha za madaktari, madaktari wote ambao hawajalipa ada zao kulingana na sheria walizojiwekea.

Alisema kama daktari hataki kulipa ada maana yake anajitoa kwenye orodha ya wataalamu hao kwa mujibu wa masharti waliojiwekea, na ndio maana anasababisha uwepo wa vishoka.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, aliwataja viongozi wa bodi hizo kuwa ni Prof. Mkongo Mlozi wa LITA, Dk. Bonaventura Baya wa MPRU na Prof. Kazwala Rudovick Baraza la Vetenari anaendelea.

Kwa upande wake, Prof. Mlozi alimshukuru waziri kwa uteuzi wao na kuahidi kuyafanyia kazi maagizo aliyotoa kwao.

Alisema timu hiyo iliyoteuliwa itaanza vikao vyake haraka ili kufanya utekelezaji wa maagizo hayo ambayo ndiyo dira ya kazi.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akizungumza wakati akizindua bodi tatu za wizara hiyo jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Waanza ujenzi shule ya kijiji

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KUTOKANA na kukosekana kwa shule ya sekondari Kijiji cha Nkulabi jijini Dodoma, wakazi wake wameanza ujenzi wa shule ili kuwaondolea wanafunzi adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 10 kufuata elimu kijiji jirani cha Mpunguzi.

Ujenzi huo ulianza jana kwa nguvu ya wananchi na kuungwa mkono vifaa mbalimbali vya ujenzi na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde.

Wakizungumza kijijini hapo wakati wa uchimbaji wa msingi wa shule hiyo ambayo itaitwa Nkulabi, wakazi hao walisema ujenzi wa shule hiyo utajibu vikwazo mbalimbali vilivyoikabili kata hiyo kwa muda mrefu, ikiwamo wanafunzi kutembea umbali mrefu.

Mkazi wa eneo hilo, Sechela Mika alisema wanamshukuru mbunge huyo kwa kusaidia ujenzi wa shule hiyo kwa kuwa watoto wao walikuwa wakirubuniwa na madereva wa bodaboda.

"Tunashukuru sana kwa msaada, watoto wetu walikuwa wanapata shida inafikia kipindi hata watoto wetu wanadanganywa na madereva badoboda, mtoto anajitoa kwa sababu anakuwa hana chochote matokeo watoto wetu wanapata mimba," alisema.

Naye Janeth Sefa, alisema watoto wao walikuwa wakipata shida kwa kutembea umbali mrefu hali, ambayo imekuwa ikiwaathiri katika masomo yao.

"Watoto wetu walikuwa wanapata shida, wanaenda mpaka Mpunguzi wanachelewa kufika shuleni," alisema.

Kwa upande wake, Mavunde alitoa mifuko 100 ya saruji, matofali pamoja na gharama za mafundi watakaojenga madarasa matatu.

Mavunde alisema ujenzi wa shule hiyo ni moja ya ahadi zake alizowahi kuzitoa, na alitoa wito kwa wananchi kuendelea kuiunga mkono serikali na viongozi wenye nia ya kuwapelekea maendeleo.

Aliwataka baadhi ya watu wanaoingiza siasa katika masuala ya maendeleo kuacha, huku akiwataka wanaotaka kugombea wajitokeze kuanzia Julai 14, mwaka huu kwa kuwa ndipo ubunge wake unakoma.

# Wenye ulemavu waiomba NEC wakalimali kwenye kampeni

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

VYAMA vya watu wenye ulemavu mkoani Dodoma, vimeiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhakikisha inaweka wakalimani wa lugha ya alama kwenye mikutano yote ya kampeni.

Rai hiyo ilitolewa na Mratibu Mkuu wa shirika la kiroho maalum kwa jamii ya watu wenye ulemavu wa kusikia mkoani Dodoma, Askofu Frank Laurent, wakati akizungumza na viongozi wa siasa, Jeshi la polisi, NEC na wenye ulemavu.

Akizungumza katika warsha ya mradi wa uboreshaji wa mazingira shirikishi na wezeshi kwa watu wenye ulemavu katika uchaguzi mkuu ulioandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la The Foundation For Civil Society, alisema makundi ya walemavu yanatakiwa kupata haki.

Alisema ili makundi ya watu wenye ulemavu wapate haki zao za msingi kwenye kampeni hizo za uchaguzi mkuu zitakazofanyika mwaka huu, NEC inashauriwa kuweka wakalimani wa lugha ya alama.

Koplo Athuman Rashidi kutoka Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwapo kwa wataalamu wa lugha ya alama katika mikutano ya kampeni ili kuwasaidia watu wasiosikia.

Pia, aliviomba vyama vya siasa, kuhakikisha vinawatengea maeneo maalum, watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali katika maeneo watakayoyafanyia mikutano yao ya kampeni zao.

Naye Ofisa Uchaguzi Jimbo la Dodoma Mjini, Albert Kasoga, alivitaka vyama vya siasa kutoa nafasi kwa makundi maalum ya watu wenye ulemavu wakati wa kuwapitisha wagombea watakaokuwa na sifa na vigezo vya kuwa viongozi.

Alisema kwenye mchakato wa kuwapata wagombea hao, vyama vya siasa ndiyo ngazi ya kwanza katika kupendekeza majina, hivyo vinatakiwa kutoa nafasi kwanza kwa makundi ya watu wenye ulemavu kwa wale wenye sifa.

Kadhalika, alivitaka vyama vya siasa, kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu wa viungo, ili kuwawezesha kushiriki vyema kwenye majukwaa watakapohitajika kuzungumzia ilani ya vyama vyao.





## Wajasiriamali Mbalizi waishukuru serikali kuondoa hofu corona

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADHI ya wajasiriamali katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, wameishukuru serikali kwa kuwatoa hofu wakati wa janga la virusi vya corona ambalo lilikuwa linatishia maendeleo ya biashara zao.

Baadhi ya wajasiriamali hao walisema walikuwa wanajiandaa kufunga biashara zao baada ya kusikia baadhi ya nchi zinawafungia wananchi wao ndani wakiamini kuwa hata Tanzania ingekuwa hivyo.

Anna Solomon, mchuuzi wa mahindi katika Soko la Tarafani Mjini Mbalizi, alisema waliingiwa na hofu ambayo ilikuwa inatishia ustawi wa biashara zao pamoja na maisha yao ambayo yanategemea utafutaji wa kila siku.

Alisema hata wanunuzi wa mazao yao ambao huwa wanatoka katika mikoa mbalimbali walianza kupungua na kusababisha hofu nyingine ya kuporomoka kwa bei ya mazao yao, lakini wakapata matumaini baada ya Rais kutangaza kuwa shughuli ziendelee.

"Kauli ya Rais ilituponya maana tulikuwa tumeanza kukata tamaa, tulikuwa tunajifikiria kwamba kama mataifa tajiri duniani yanafungua watu wao ndani hata sisi tatizo hilo lingetukumba na kutuharibia mtiririko wa maisha," alisema Anna.

Alisema kutokana na ugonjwa huo, walikuwa wanafuatilia taarifa kwenye vyombo vya habari na waliposikia baadhi ya shughuli kuanza kufungwa zikiwamo shughuli za michezo na taasisi za elimu waliamini kuwa hata biashara zingefungwa.

Naye Jonas Dembe, alisema baada ya serikali kuwataka waendelee na biashara zao kwa tahadhari, walihamasishana na kuwekeana mikakati ya kila mmoja kuweka maji ya kunawa mikono kwenye ofisi yake ili kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema tahadhari ya ugonjwa huo bado wanaendelea japo baadhi ya wananchi wameanza kupunguza hofu, na kuacha kuchukua tahadhari kutokana na ugonjwa huo kupungua.

# BAWACHA yamchukulia Sugu fomu kutetea ubunge

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BARAZA la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) Wilaya ya Mbeya Mjini limemchukulia fomu za kugombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Joseph Mbilinyi 'Sugu' likidai ndiye mwenye uwezo wa kulitetea.

Akizungumza wakati wa kumkabidhi fomu hizo, Mwenyekiti wa BAWACHA, Wilaya, Elizabeth Mwakimomo, alisema wanawake wa Mbeya Mjini waliamua kuungana na kuchangishana fedha za kuchukulia fomu hizo kutokana na kuridhishwa na mambo ambayo mbunge huyo amewafanyia wananchi wa jimbo hilo na taifa.

Alisema Sugu ndiye mbunge aliyesaidia kutetea wananchi ili gharama za kuhifadhi maiti kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti hospitalini ziondolewe, na akafanikiwa na hivyo kuwaletea nafuu wananchi ambao walikuwa wanaingia gharama kubwa.

Vilevile, alisema Sugu ambaye ni msanii wa nyimbo za kizazi kipya (Hip Hop), amesaidia kusomesha watoto yatima zaidi ya 500 wa Jimbo la Mbeya Mjini, ambao kwa sasa wamefikia katika ngazi tofauti za elimu nchini, na kwamba mchango huo umesaidia kuwakomboa watoto hao.

"Sisi kama kinamama tumeguswa na michango yake, hivyo tumeamua kumtuma tena akatuwakilishe kulitetea jimbo na wale wote wanaozunguka zunguka kwenye jimbo wajue kuwa 'Sugu' ndiye mwenye jimbo," alisema Mwakimomo.

Aliwataka wananchi wa jimbo hilo kuendelea kuungana na kumwamini kiongozi wao huyo kwa maelezo kuwa ndiye kiongozi mwenye uwezo wa kuwatetea wananchi.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa fomu hiyo, Sugu aliwashukuru wanawake hao kwa kumwamini na kuamua kumuomba agombee tena kwa maelezo kuwa kitendo walichofanya ni cha ujasiri na kinaonyesha imani yao kwake.

Alisema uamuzi wa wanawake hao unatoa majibu kuwa kiongozi huyo anaungwa mkono na makundi mbalimbali ya kijamii tofauti na ambavyo wapinzani wake wamekuwa wakiamini kuwa anakubalika na 'masela' wa stendi.

Alisisitiza kuwa wanawake hao wamemsaidia kupunguza gharama ambazo alitakiwa aingie mwenyewe za kwenda kulipia fomu hizo ambazo zinachukuliwa kwa gharama ya Sh. 100,000.

"Nilipoambiwa mnaondoka nimeamua kumwomba mlinzi afunge mlango ili nipate nafasi ya kuongea nanyi, sasa nikiwaangalia naona wapo wadogo zangu, dada zangu, shangazi zangu, bibi zangu na mama zangu, hii inaonyesha kuwa ninakubalika na rika zote," alisema Sugu.

Alisema kutokana na kuungwa mkono na wanawake hao, ana uhakika kuwa pamoja na upinzani ambao utajitokeza, lakini atatoboa na kuliongoza jimbo hilo kwa miaka mingine mitano.

Sugu amekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini kupitia CHADEMA kwa miaka 10, ambapo awamu ya kwanza aliingia mwaka 2010 akimgaragaza aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Benson Mpesya (CCM) ambaye aliongoza miaka 10.



Aliyekuwa Mbunge wa a Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (kulia), akipokea fomu ya kugombea ubunge wa jimbo hilo, kutoka kwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), Wilaya ya Mbeya Mjini, Elizabeth Mwakimomo, nyumbani kwake juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC aheshimu ushauri wa JPM

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametangaza kusitisha nia yake ya kwenda kugombea ubunge katika Jimbo la Iringa Mjini na kuamua kubakia na wadhifa wake wa ukuu wa mkoa wa Mbeya.

Uamuzi wa Chalamila unatokana na maelekezo ya Rais John Magufuli wa kuwataka wateule wake kutekeleza majukumu aliyowapa badala ya kwenda kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi kwa lengo la kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ukiwamo ubunge.

Akizungumza na wanahabari jijini Mbeya, Chalamila alikiri kuwa na mpango wa kwenda kugombea ubunge Iringa Mjini, lakini akasema kuwa ameamua kusitisha nia hiyo na kuendelea na majukumu yake ya ukuu wa mkoa ikiwamo kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa mkoani Mbeya.

"Ukweli ni kwamba nilidhamiria kwenda kugombea ubunge katika Jimbo la Iringa Mjini, na ninawahakikishia kuwa ningeshinda asubuhi na mapema, lakini nitakuwa mtovu wa nidhamu kama nitakwenda kugombea, huku nikiwa namkwaza mwenyekiti wangu wa CCM ambaye ni Rais wa nchi yetu," alisema Chalamila.

Chalamila alisema kuwa katika kipindi kifupi kilichopita, Rais Magufuli ametoa fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani Mbeya, ambayo inahitaji usimamizi wa karibu ili zifanye kazi iliyokusudiwa.

Alisema hivi karibuni serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 14 kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, kuna fedha zimetumwa zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mpya ya Mkuu wa Mkoa na fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya barabara, miradi ambayo inahitaji usimamizi wa karibu.


Chalamila pia alisema analo jukumu la usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya serikali mkoani Mbeya, ambalo anapaswa kuendelea kulisimamia badala ya kwenda kugombea ubunge.

"Wakati naingia hapa Mbeya, makusanyo ya serikali yalikuwa shilingi bilioni saba, lakini sasa hivi tunakusanya zaidi ya asilimia 103 ya lengo la shilingi bilioni 12 ambalo tulikuwa tumepangiwa kukusanya, hivyo nitakuwa mtovu wa nidhamu kuyaacha haya nikaenda kugombea ubunge kinyume cha maelekezo ya Rais," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa pia serikali imetuma kiasi cha Sh. milioni 795 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Mbeya Day na juzi zilitumwa shilingi milioni 752 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Rungwe ambazo zote zinahitaji usimamizi wake.

"Unapomsikiliza Rais unaiona mantiki yake kwamba fedha zote hizi zinapotumwa mahali ambapo hakuna mhasibu, hakuna mhazini, hakuna msimamizi... wote mmeondoka mmekwenda kugombea mnasababisha vilio vikubwa kwa Watanzania, sasa ni busara sana unaposikia ushauri wa wakuu ni vema kuutekeleza," alisema Chalamila.

"Kwa maelezo hayo nitamke tu kwamba ile nia yangu ya kwenda kugombea ubunge pale Iringa Mjini...sasa nimeiondoa na sasa nitaendelea kuchapa kazi nikitekeleza majukumu yangu ya kuwahudumia wananchi kama Mkuu wa Mkoa wa Mbeya."





# ZAECA yatoa tahadhari rushwa Uchaguzi Mkuu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAMLAKA ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), imewataka wananchi kuchagua viongozi wazalendo wenye lengo la kuleta maendeleo na wasikubali kurubuniwa kwa rushwa.

Ofisa wa ZAECA, Sada Salum, aliyasema hayo jana alipozungumza na viongozi wa Jimbo la Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja ili kuwajenga uwezo viongozi hao kujua athari za rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Alisema hiki ni kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu ambacho wanachama mbalimbali huomba nafasi za uongozi, huku wengine wakitumia rushwa kurahisisha upatikanaji wa matakwa yao.

Alisema wapo viongozi ambao hawakutekeleza majukumu yao vizuri na wanachotaka kufanya ni kutumia rushwa ili kupenya tena katika kinyang'anyiro hicho.

Issa aliwataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wasikubali kuchagua viongozi wa majimbo kwa ushawishi wa rushwa kwa kuwa kitendo hicho ni kosa kwa mujibu wa sheria.

"Mamlaka (ZAECA) ipo macho kupambana na viongozi watakaojishughulisha na kutoa rushwa kwa lengo la kupitishwa katika uongozi wa majimbo," alisema.

Mjumbe wa Kamati ya Jimbo la Mahonda katika mkutano mkuu, Juma Jongo, alisema wamejipanga vizuri kuepukana na rushwa kupitia viongozi wa majimbo katika nafasi ya uwakilishi, ubunge, udiwani na hata uchaguzi wa taifa. Alisema madhara ya kuchagua viongozi kwa misingi ya rushwa yameonekana, akibainisha kuwa yapo baadhi ya majimbo wanachama wake walichagua viongozi kwa misingi hiyo na wameshindwa kupata maendeleo waliyotarajia.

"Tunakipongeza chama chetu cha CCM katika mwaka huu suala la kupambana na rushwa limepewa kipaumbele cha kwanza kuanzia ngazi ya chini hadi taifa, Mwenyekiti wetu, Rais John Magufuli amekuwa mstari wa mbele kukemea rushwa," alisema.

Mjumbe wa mkutano mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Fatuma Ali, alisema wanawake kamwe hawakubali kurubuniwa kuchagua kiongozi kwa misingi ya rushwa kwa sababu athari zake ni kubwa.

"Sisi wanawake tupo makini katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, hatukubali kupokea ushawishi wenye mwelekeo wa rushwa kwa maslahi ya wachache, tunataka maendeleo," alisema.



Aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Mohamed Raza, akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, wakati akitangaza nia ya kugombea tena uwakilishi katika jimbo hilo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# DC aonya wavamizi msitu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Rajab Ali, amepiga marufuku wananchi na wakazi wa Kijiji cha Kiwengwa kufanya shughuli za kilimo katika msitu wa hifadhi ambao umeanza kuvamiwa.

Alisema hayo jana alipotembelea Msitu wa Hifadhi ya Kikwengwa baada ya kupata taarifa za uvamizi unaofanywa kwa lengo la kupata maeneo ya shughuli za kilimo na kukata kuni.

Kiwengwa alisema msitu huo uko katika orodha ya misitu ambayo inatakiwa kulindwa ili kuhifadhi mazingira.

Alipiga marufuku shughuli za kilimo katika msitu huo baada ya kubaini kuwa baadhi ya watu wamejipenyeza na kuanza kufanya uharibifu ikiwamo kukata kuni na kuanza kujenga majengo kwa ajili makazi.

"Serikali ya Wilaya ya Kaskazini B inapiga marufuku mara moja shughuli zote za kijamii katika Msitu wa Hifadhi ya Kiwengwa ikiwamo ujenzi wa nyumba na kilimo," alisema.

Wajumbe wa Kamati ya Msitu wa Hifadhi ya Kiwengwa, wamepongeza uamuzi wa kuzuiwa kwa shughuli ndani ya msitu huo kutokana na kujitokeza kwa athari mbalimbali ikiwamo ukataji wa miti.

Juma Ali, mjumbe wa kamati hiyo, alisema wapo watu tayari wamejiingiza katika msitu huo na kuanza kuweka makazi ya kudumu.

Alisema baadhi ya watu hao wanatumia kisingizio cha kuishi katika msitu huo na kufanya matukio yanayokwenda kinyume cha sheria za hifadhi zilizoweka katika msitu huo.

"Tumefurahishwa na tamko la mkuu wa wilaya kupiga marufuku mara moja shughuli zote zinazofanywa na binadamu ndani ya msitu huu. Yapo matukio mengi ya hujuma yanayofanywa na wananchi," alisema.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeshautangaza msitu huo kuwa katika orodha ya hifadhi ya taifa mwaka 2007 kwa lengo la kulinda rasilimali zilizomo katika msitu huo ikiwamo vyanzo vya maji.

## Ofisi ya Rais yataja manufaa ya ugatuzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema lengo la ugatuzi ni kufikisha huduma muhimu za kijamii kwa wananchi moja kwa moja na kuleta maendeleo.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais anayeshughulikia tawala za mikoa, Khalid Abdalla, aliyasema hayo jana wakati akikabidhiwa hospitali iliyokuwa ikimilikiwa na Shirika la Kimataifa la Kijiji cha Kulea Watoto (SOS) huko Mombasa nje kidogo ya Mji wa Zanzibar.

Alisema serikali imegatua huduma muhimu za kijamii kwenda moja kwa moja kwa wananchi ikiwamo elimu ya msingi na maandalizi, afya ya msingi pamoja na kilimo, ili kurahisisha upatikanaji wa maendeleo.

Alisema huduma za afya ya msingi zitaendelea kutolewa bure kwa wananchi wote licha ya kugatuliwa ili wananchi waondokane na tatizo la maradhi.

"Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa inakipokea kituo cha afya kilichokuwa kikimilikiwa na Shirika la Kimataifa la Vijiji vya Kuleya Watoto (SOS) ...tunaahidi kukitunza kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi wanaoishi jirani na eneo hili," alisema.

Aliongeza kuwa kituo hicho kitakuwa na huduma zote za kinamama wajawazito na watoto na kuwataka wanawake kuzitumia huduma hizo ili ya kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

"Bado tunakabiliwa na tatizo la vifo vya kinamama na watoto kwa sababu baadhi yao hawazitumii vizuri huduma zinazotolewa na hospitali zetu," alisema.

Mkurugenzi wa Kijiji cha SOS, Asha Seif, alisema kituo hicho kimepelekwa katika Serikali za Mitaa kupitia ugatuzi ili kuleta ufanisi wa huduma za afya kwa makundi yote ikiwamo kinamama wajawazito.

Alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 1991 na kuanza kutoa huduma kwa watoto pamoja na wananchi wanaoishi maeneo ya jirani na ilipofika mwaka 2007 kilifanyiwa ukarabati mkubwa kwa lengo la kutoa huduma mbalimbali zikiwamo za kinamama wajawazito.

"Kituo cha Afya cha Kijiji cha Kimataifa cha SOS Zanzibar sasa tunakipeleka moja kwa moja katika halmashauri ya tawala za mikoa kwa lengo la kutoa huduma kwa wananchi wa eneo hili na majirani zao," alisema.

Sheha wa Shehia ya Mombasa, Hussein Abrahman, alisema wamefarijika kukabidhiwa kituo hicho ambacho kitatoa huduma kwa wananchi wa Manispaa ya Magharibi B Unguja na hivyo kusaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha huduma za afya kwa makundi mbalimbali, hasa kinamama wajawazito na watoto.

"Nimekipokea kituo hiki ambacho kitakuwa na uwezo wa kutoa huduma zote muhimu za afya ikiwamo kwa kinamama wajawazito na watoto. Haya ni mabadiliko makubwa na tunawaomba wananchi wazitumie huduma hizi kikamilifu," alisema.

# Chanzo uzalishaji duni wa pareto chaanikwa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKATI Tanzania ikiwa ya kwanza duniani kwa uzalishaji bora wa pareto, zao hilo halijapewa umuhimu wa kutosha kutokana na kiwango cha uzalishaji kuwa chini, imebainika.

Sababu kubwa inayokwamisha uzalishaji huo imeelezwa kuwa ni kukosekana kwa fedha za utafiti za uzalishaji wa mbegu bora.

Mtafiti wa Pareto kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Uyole mkoani Mbeya, Baraka Mvile, alisema alipozungumza na Nipashe kuwa ulizalishaji wa pareto nchini kwa sasa unafikia tani 2,000 mpaka 3,000 wakati mahitaji bado ni makubwa.

Alisema inakadiriwa mahitaji ya pareto duniani ni tani 16,000 na bei imekuwa ikipanda kwa kasi kutokana na zao hilo kutumika kwa ajili ya kuzalishia dawa za kuulia wadudu wa mimea na wale wa nyumbani kama mbu.

Licha ya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kwa uzalishaji bora wa pareto, alisema ni nchi ya pili kwa ukubwa na ya kwanza ikiwa Australia inayozalisha zao hilo kwa wastani wa 8000 kwa mwaka, lakini haijaifikia ubora wa Tanzania kutokana na nchi hiyo kutumia mashine katika uvunaji ambayo inapunguza ubora.

Mvile alisema changamoto kubwa katika utafiti wa uzalishaji mbegu bora ni rasilimali fedha ambazo kwa sasa tegemeo lao kubwa ni kiwanda cha pareto kilichoko Mafinga mkoani Iringa. Soko kubwa la pareto katika kiwanda hicho ni Marekani.

Naye Mkuu wa Idara ya Mazao wa TARI Uyole, Daud Mbongo, alisema uzalishaji huo uko chini kutokana na wakulima wengi kutumia mbegu za kizamani ambazo hazina tija.

Alisema ili kuongeza uzalishaji wa zao la pareto nchini, kunahitajika serikali kukiwezesha kituo hicho kuzalisha mbegu za kisasa ili zisambazwe kwa wakulima.

Mbongo alisema zao hilo ni maalumu kwa ajili ya kutengeneza dawa mbalimbali zinazoua wadudu shambani, ghalani, nyumbani na kwenye mifugo, hivyo linapaswa kupewa kipaumbele ili kuliingizia taifa fedha za kigeni.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema pareto ni zao la pekee linalotoa kiuatilifu ambacho ni rafiki wa mazingira ambacho hakina madhara kwa mtumiaji na kuliongezea thamani zao hilo.



Baadhi ya vijana wanaolelewa na Shirika la SOS Children's Villages Tanzania, wilayani Nyamagana, mkoani Mwanza, wakishona vikapu kituoni hapo, jana, ukiwa ni mradi wao wa ujasiriamali unaowawezesha kupata kipato. **PICHA: ROSE JACOB**

# Bima za NMB zachangamkiwa Sabasaba

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wengi wa Jiji la Dar es Salaam, wamechangamkia huduma za bima zinazotolewa na Benki ya NMB kwenye maonyesho ya Sabasaba ya mwaka huu.

Benki hiyo imesema hatua hiyo imechangiwa na jamii kupata elimu stahiki na kudhihirisha kuwa hawana tatizo na suala la kukata bima kwa ajili ya uhakika wa maisha na usalama wa mali zao.

Aidha, imeeleza kuwa hali hiyo pia imechangiwa na ubunifu wake kama ilivyo huduma mpya ya bima ya benki hiyo ambayo kibiashara inajulikana kwa jina la NMB Bancassaurance.

Viongozi wa benki hiyo pamoja na wataalamu wa NMB Bancassurance walisema mvuto wa huduma hiyo umekuwapo tangu siku ya kwanza ya maonyesho ya mwaka huu ambayo kilele chake kilikuwa jana.

"Sikuwahi kuwa na wazo la kukata bima maishani mwangu, lakini baada ya kufika hapa leo na kuelimishwa kuhusu huduma hii, nimebadilika kabisa. Ngoja nikajipange lazima niwe na bima hasa hii ya elimu ya watoto wangu nikiwa hai au nimekufa," alisema Zawia Omari, mkazi wa Bungo-Kibaha, baada ya kutembelea banda la NMB jana.

"Kitu kingine kikubwa nilichokigundua kumbe ni zaidi ya banda la maonyesho kwa sababu kila huduma inapatikana humu ndani," aliongeza Zawia.

Meneja wa Tawi la NMB la Temeke, Kidawa Masoud, alisema hilo limechangiwa na moja ya mikakati yao ya ushiriki wa mwaka huu ya kuwa na mabalozi wa NMB Mkononi ambao ni vijana maalumu wa benki hiyo waliondaliwa kwa ajili ya kusaidia usajili wa watu, ili waweze kutumia huduma hiyo na kutoa elimu kuhusu faida na manufaa yake.

"Tayari tumesajili watu wengi na kuwaelimisha wengi zaidi. Umaarufu wa NMB Mkononi umetokana na uwezo wake wa kumwezesha mteja kufanya miamala mbalimbali akiwa mahala popote pale alipo bila kufanya safari ya kwenda benki," Kidawa alifafanua.

Meneja wa NMB Wakala, Edwin Kisamo, alisema shughuli mojawapo kubwa ni kusaidia kukusanya mapato ya serikali wakati wa maonyesho kutoka vyanzo mbalimbali kama vile mabanda ya NIDA, RITA, TRA na Tantrade inayoandaa maonyesho haya.

## Rai vituo vya utafiti kufikisha matokeo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Geoffrey Mkamilo, amevitaka vituo vya utafiti nchini kufikisha matokeo ya utafiti na teknolojia wanazozizalisha kwa wakulima.

Mkamilo, alitoa wito huo hivi karibuni katika sherehe za uzinduzi wa Siku ya Mkulima zilizofanyika katika kituo cha utafiti wa miwa ya sukari kilichopo mjini Kibaha (TARI-Kibaha).

Alisema, lengo la utafiti huo ni kuhakikisha wanawasaidia wakulima na wadau mbalimbali kupata elimu ya namna bora ya uzalishaji hivyo ni vyema matokeo ya utafiti yakawafikia wakulima kwa wakati.

"Kama utafiti unaofanywa hautawafikia wakulima ni wazi kuwa hakutakuwa na umuhimu wa kuwapo kwa vituo hivyo jambo ambalo litarudisha nyuma maendeleo ya kilimo hapa nchini kwani hakutakuwa na mabadiliko," alisema.

Alisema ofisi yake itahakikisha inaongeza nguvu zaidi katika vituo hivyo ili teknolojia hizo ziwafikie wakulima kwa ajili ya kuleta matokeo chanya.

Aliishukuru serikali kwa kutatua baadhi ya changamoto zilizokuwa zikikabili vituo vya utafiti nchini na kwamba kwa sasa wanaendelea kufanyakazi vizuri.

Kwa upande wake Meneja wa kituo cha utafiti wa miwa kilichopo Kibaha, Dk. Heldelitha Msita, alisema katika kipindi cha miaka mitano kituo chake kimepata mafanikio makubwa.

## NCBA kuanza kutoa huduma leo

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya NIC Tanzania na CBA zinatarajia kuanza kutoa huduma kama Benki ya NCBA kuanzia leo.

Katika kukamilisha maandalizi ya kuanza kutoa huduma, wajumbe wa bodi, wamemteua Magret Karume, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa benki ya NIC, kuwa Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mkuu Mtendaji wa benki ya NCBA.

Mwenyekiti Mteule wa Bodi ya NCBA, Sharmapal Aggarwal, aliyaeleza hayo juzi wakati akidhibitisha uteuzi huo na kumepongeza Karume kwa kuteuliwa kwake.

"Tunatambua uzoefu wake mkubwa kwenye sekta ya benki na tunamsifu kwa kujitoa kwake upya kwenye benki. Tunaamini kuwa yeye ni mtu sahihi kuiongoza Benki ya NCBA kwenye zama mpya ya maendeleo endelevu na kuleta mafanikio kwa wadau wote Tanzania na bara la Afrika kwa ujumla," alisema Aggarwal.

Alisema nafasi yake itaiongoza benki ya NCBA kwenye biashara za kidijitali ambayo ni kiini cha ukuaji endelevu wa biashara ya kundi hilo wakati ikilenga kuwa benki inayoongoza kwenye kanda katika miaka mitano ijayo.

Alisema kuunganishwa kwa benki zote mbili imewezesha kukua na kuwa benki kubwa katika sekta ya digitali.

# Sababu Kwanza TV kufungiwa

**Na Mary Geofrey**

KAMATI ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imekifungia kituo cha Kwanza Online TV kutokutoa huduma kwa kipindi cha miezi 11 kuanzia juzi, kwa kukiuka kanuni za utangazaji kwa kuchapisha taarifa inayodaiwa kutolewa na ubalozi wa Marekani nchini Tanzania.

Kamati hiyo imesema Online TV imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018 na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui ya TCRA, Joseph Mapunda, alitangaza hukumu hiyo jijini Dar es Salaam.

Alisema baada ya kupitia kwa umakini na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi wa maandishi uliotolewa na uongozi wa Kwanza Online TV, kamati hiyo iliridhika pasi na shaka kuwa Kwanza Online TV kupitia ukurasa wake wa mitandao ya kijamii wa Instagram imekiuka Kanuni Na. 7(1) (a), (b) na 12 (l) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni) ya mwaka 2018.

"Pia amekiuka Kanuni Na. 11(1)(a) na 15(2)(b) na (c) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

"Hivyo basi, kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2017, tumewafungia kutoa huduma kwa muda wa miezi 11 kuanzia leo (jana)," alisema Mapunda.

Akifafanua kuhusu kosa walilofanya, alisema Julai Mosi, mwaka huu, kituo hicho kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii (Instagram), kilikiuka Kanuni za Utangazaji kwa kuchapisha taarifa inayodaiwa kutolewa na ubalozi wa Marekani nchini Tanzania.

Alisema Kwanza Online TV ilichapisha taarifa hiyo iliyojaa upotoshaji kwa jamii bila kutafuta usahihi na ukweli wa taarifa husika, na bila ya kuzingatia mizania ya habari. Alisema ilichapisha maudhui hayo yaliyokuwa katika mfumo wa picha mnato, ambayo yanadaiwa yanatoka Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania.

Mapunda alisema katika utetezi au maelezo ya kimaandishi yaliyowasilishwa mbele ya kamati hiyo, uongozi wa Kwanza Online TV uliiambia kamati kuwa, inapinga mashtaka husika kwa sababu imetoa taarifa inayotimiza matakwa ya Katiba ya nchi chini ya Ibara ya 18, inayompa mtu uhuru wa kutoa maoni yoyote, kutoa mawazo yake, kutafuta, kupokea, kutoa habari na dhana zozote kupitia chombo chochote bila kujali mipaka ya nchi.

# Muroto aonya wanaoibia abiria kutumia dawa za wagonjwa akili

**Renatha Msungu,** DODOMA

WAKATI Jeshi la Polisi mkoani Dodoma, likiendelea na msako wa wahalifu, wezi wa magari wamekuja na mbinu mpya ya kutumia vidonge vya watu wenye ugonjwa wa akili na kuwapa abiria katika mabasi ili kuwaibia.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Gilles Muroto, alisema wezi hao wanaposhindwa kuiba magari wanahamia katika mabasi na kutumia dawa hizo kuweka kwenye biskuti ili kuwalewesha wasafiri na baadaye kuwaibia.

Alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha linawasaka wezi wa aina hiyo ikiwamo kuwachukulia hatua kali za kisheria.

"Naomba jamii iwe makini wezi wanabuni mbinu mpya kika kukicha ili kuwaibia watu," alisema Muroto.

Alisema popote walipo Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na mikoa jirani imejipanga kuwasaka wahalifu wote wanaojipanga kuichafua makao makuu.

Katika hatua nyingine jeshi hilo limewakamata watuhumiwa wawili ambao walifanya matukio mbalimbali ya wizi na unyang'anyi wa magari ya ndani na nje ya nchi.

Kamanda Muroto, alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakiwapa madawa ya kulevya abiria katika mabasi yaendayo mikoa mbalimbali hapa nchini kwa kutumia biskuti.

Alisema kuwa katika oparesheni hiyo walikamata silaha mbili aina ya pisto na silaha aina ya Browning yenye namba A373810 na risasi 14 inayomilikiwa na Jumbe Kamugisha (46), mkazi wa Chanika Msongola, jijini Dar es Salaam.

"Pia alikutwa akiwa na vidonge 124 aina ya Rolvan na pakiti moja ya biskuti wanazotumia wahalifu hao kuwalewesha abiria kwenye mabasi," alisema.

Pia silaha ya pili ni aina ya Browning yenye namba BO87111 na risasi 15 inayomilikiwa na George Semtego (36), mkazi wa Mbezi Beach jijini Dar es Salaam, mfanyabiashara.

"Silaha hizi zinamilikiwa kihalali, lakini zimekuwa zinatumika katika matukio ya uhalifu na kuongeza kuwa uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa hawalipii, lakini pia hazikuhakikiwa na kupewa namba za silaha za hapa nchini," alisema Muroto.

Kamanda alitoa wito kwa wanaomiliki silaha na kutumia katika vitendo vya uhalifu wote kuchukuliwa hatua na kushtakiwa.



Mbunge wa Bunda Mjini, mkoani Mara, Ester Bulaya (kwenye gari), akisalimiana na wakazi wa Bunda, alipowasili jimboni humo juzi, akitokea jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kairuki ahamasisha kilimo cha pamoja

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Angela Kairuki, ameutaka uongozi wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, kuhamasisha wananchi kulima kilimo cha pamoja, hususani mazao yenye uhitaji mkubwa katika viwanda ili kuwezesha kilimo chenye tija na upatikanaji wa masoko ya uhakika.

Alitoa rai hiyo wakati wa ziara yake ya kikazi wilayani humo na kusema kilimo cha pamoja kina manufaa makubwa kwa wakulima kwa kuwa wawekezaji watanunua mazao mengi kwa pamoja na kuinua uchumi.

Alisema, yapo mazao yenye uhitaji mkubwa katika viwanda mbalimbali nchini na kutoa mfano wa zao la mtama kwamba kiwanda kimojawapo cha KBL kilichopo wilayani Mwanga kina mahitaji ya zaidi ya tani 6,000.

"Wilaya ya Same ina fursa nyingi za kilimo kutokana na ardhi yake kuwa na uwezo wa kustawisha mazao ya aina nyingi tofauti na maeneo mengine, kwani yapo maeneo ya umwagiliaji wanaweza kulima kilimo cha umwagiliaji na maeneo mengine makubwa ya kilimo kingine, hivyo hamasisheni kilimo cha pamoja chenye tija," alisema Kairuki.

Aliutaka pia uongozi wa wilaya hiyo, kushughulikia migogoro ya ardhi hususani inayohusu wananchi na wawekezaji kwa haraka, ili kutoa muafaka na kuwezesha uwekezaji kuendelea kwa tija.

"Mwekezaji anapofika mahali akakutana na migogoro, inamchelewesha kuanza kazi zake, lakini inakwamisha kasi ya uwekezaji, hivyo hakikisheni mnashughulikia migogoro kwa haraka iwezekanavyo, ili kupanua wigo wa uwekezaji."

Katika hatua nyingine, Kairuki alitaka kuangaliwa uwezekano wa kuanzishwa machinjio ya kisasa, katika wilaya hiyo, akieleza kuwa ipo mifugo mingi na endapo itaanzishwa machinjio, itakuwa fursa nzuri ya uwekezaji katika halmashauri hiyo.

"Suala la kuanzisha machinjio, liende sambamba na upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, pamoja na kutoa elimu kwa wafugaji juu ya umuhimu wa machinjio ili kuwawezesha kuitumia na kuleta tija kwa wilaya," alisema Kairuki.

Alitaka pia wilaya hiyo kujenga makumbusho ya madini, ambayo watalii pamoja na wananchi watatembelea na kujionea madini mbalimbali ambayo yanapatikana wilayani humo.

"Fursa ya madini ni kubwa katika wilaya hii, sasa wekeni mkazo kwenye utafiti ikiwezekana iwe kijiji kwa kijiji na kuwapo na maduka ya kuuzia vifaa vya uchimbaji ikiwamo baruti."

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema wakulima kulima zao moja katika eneo moja, itawarahisishia wanunuzi kupata mazao wanayohitaji kwa wingi na hivyo kuwa na masoko ya uhakika.

# ALLEGRI AZUNGUMZIA KUTAKIWA MADRID



**TURIN,** Italia

MASSIMILIANO Allegri amesema alikuwa na mawasiliano na Real Madrid juu ya kuwa kocha wao mkuu miaka miwili iliyopita, lakini alitaka kubakia Juventus.

Kocha huyo wa zamani wa AC Milan alitumia misimu mitano ya mafanikio pale Juve kabla ya kuondoka mwishoni mwa msimu uliopita.

Baada ya Zinedine Zidane kuondoka Madrid baada ya msimu wa 2017-18, klabu hiyo ilikaa kwa muda mfupi na Julen Lopetegui na Santiago Solari.

Allegri alionekana kuwa mmoja ya chaguo la kikosi hicho na Muitaliano huyo alimshukuru Rais wa Real Madrid, Florentino Perez kwa kuwa na nia nae kipindi hicho.

Madrid walirudi tena kwa Zidane Machi mwaka 2019.

"Miaka miwili iliyopita, kulikuwa na mawasiliano, lakini hakuna kilichofanyika kwa sababu nilikuwa na mkataba na Juve," alisema Allegri akiliambia gazeti la Marca.

"Zaidi ni kwamba, nilikuwa na majukumu muhimu zaidi na klabu pamoja na mashabiki wake."

Allegri alipoulizwa nini anachokipenda kwa kazi anayoifanya Zidane pale Santiago Bernabeu, huku wakiwa kwenye nafasi nzuri ya kulitwaa taji la LaLiga msimu huu 2019-20, alijibu: "Uwezo wake wa kuimarisha timu na kuwa na uwiano mzuri."

"Kwa upande wangu, nafasi ya Casemiro inaonekana zaidi kwenye kikosi kile chini ya Zizou."

# Rodgers: Arteta ameibadilisha Arsenal

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amekuwa na wakati mzuri kupunguza presha pale Arsenal na ameonyesha "ujasiri" katika miezi yake ya mwanzo klabuni hapo, amesema Brendan Rodgers.

Arsenal imeshinda mechi nne mfululizo kwenye mashindano yote kabla ya jana Juamnne kuwavaa Leicester City mchezo uliopigwa kwenye dimba la Emirates na kocha wake, Rodgers ameonyesha kukunwa na kiwango cha Arteta.

"Nafikiri Mikel amefanya vizuri sana tangu atue klabuni pale," alisema Rodgers ambaye kikosi chake kinapambana kumaliza kwenye tatu bora katika msimamo huo.

"Alikwenda kwenye klabu huku akiwa na matarajio makubwa, kitu ambacho alikijua kwa sababu alikuwa mchezaji pale.

"Amekwenda kwenye kazi yake ya kwanza, huku akipewa jukumu zito, na nafikiri anajua namna ya kudili na presha ya timu.

"Kwenye suala la ufundi na kiwango cha timu, amefanya makubwa zaidi, kwani vijana wake wanacheza soka ambalo unapenda kulitazama. Wana staili inayovutia dimbani."





# *Pulisic yupo vizuri, Hazard alifanya mengi - Lampard*

**LONDON,** England

CHRISTIAN Pulisic anacheza staili ya soka la moja kwa moja kuliko Eden Hazard, lakini anatakiwa kufikia kiwango kilichoonyeshwa na nyota huyo wa Ubelgiji wakati akicheza hapo Chelsea, kwa mujibu wa Frank Lampard.

Pulisic mchezaji wa kimataifa wa Marekani amekuwa akifurahia muda wake kwenye Ligi Kuu ya England baada ya kurudi tena, akifunga mabao kwenye ushindi dhidi ya Aston Villa na Manchester City na akapiga moja wakati wakiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Watford Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ameonyesha kuwa ana kasi nzuri kwenye nafasi yake ya ushambuliaji wa pembeni akilinganishwa na Hazard, ambaye alihamia kule Real Madrid mwaka jana baada ya misimu saba ya mafanikio kule Stamford Bridge.

Lampard mara kwa mara amekuwa akiepuka kumlinganisha Pulisic dhidi ya Hazard na kuchambua tofauti za viwango vyao wachezaji hao wawili wakati akizungumza kulekea mchezo wa jana Jumanne dhidi ya Crystal Palace.

"Nikiwa nimecheza na Eden na kuona kwamba alikuja klabuni wakati akiwa na umri mdogo, sawa na Christian, tunamuona akiimarika," alisema Lampard ambaye ni mfungaji wa wakati wote wa Chelsea, ambaye alicheza na Hazard wakati akiwa kijana msimu wa 2012-13 na 2013-14.

"Anakipaji cha aina yake na yuko haraka kupokea mpira, kumiliki na kutoa pasi kwa wenzake. Anaweza kuwachezesha wachezaji wenzake.

"Alikuwa mchoyo, lakini sasa anaweza kutoa pasi za mwisho mara nyingi sana."

# Matic apewa miaka mitatu Man United

**MANCHESTER,** England

NEMANJA Matic amesaini mkataba mpya na Manchester United utakaomweka hapo hadi mwaka 2023.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia, Matic alibakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa.

Lakini klabu hiyo ilitangaza Jumatatu kwamba, mchezaji huyo amesaini mkataba mpya baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia zaidi chini ya Ole Gunnar Solskjaer.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alijiunga na United akitokea Chelsea mwaka 2017 na amecheza mechi 114.

"Nina furaha kwamba nitaendelea kuwa sehemu ya klabu hii kubwa," alisema kiungo huyo katika taarifa yake.

"Kama mchezaji, bado nina mambo mengi ya kuipa na kufanikiwa na kwenye maisha yangu ya soka nataka kufanya kitu kikubwa na Manchester United ili kuwa na heshima kubwa."

Matic ameanza katika kila mchezo kwenye mechi tatu zilizopita za United kwenye Ligi Kuu, na kuwasaidia kuendeleza wimbi la ushindi katika mechi 16 kwenye mashindano yote.

Kikosi hicho cha Solskjaer kimejivuta hadi nafasi ya tano kwenye msimamo, pointi tatu nyuma ya wanaoshika nafasi ya tatu Leicester City na kikiwa kwenye mbio za kuwania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.





# KANTE AIPA PIGO CHELSEA

**LONDON,** England

CHELSEA itakuwa bila ya N'Golo Kante kwa wiki kadhaa baada ya kiungo huyo wa Ufaransa kuumia nyonga.

Kante aliukosa mchezo wa jana Jumanne wa Ligi Kuu dhidi ya Crystal Palace na anatarajiwa kuwa nje ya dimba kwa wiki kadhaa.

Kante pia anatarajia kuwa nje ya dimba kwenye mchezo wa wikendi inayokuja dhidi ya Sheffield United, ingawa kocha wake, Frank Lampard hatarajii kama atakaa kwa muda mrefu sana nje ya dimba kutokana na maumivu hayo.

"Kante anaweza asiwe kwenye kikosi chetu kwa muda, ameumia nyonga," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilimuona alivyouguliwa, hivyo tunatarajia hatakaa nje ya dimba kwa zaidi ya wiki mbili au zaidi.

"Najua tutacheza mchezo mmoja au miwili bila yeye, lakini tunatarajia kwamba anaweza kuwa uwanjani baada ya wiki."

# *Arsenal watakiwa kumwongezea mkataba Alexandre Lacazette*

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema klabu hiyo lazima izungumze na Alexandre Lacazette kuona kama fowadi huyo anataka kusaini mkataba mpya.

Mkataba wa sasa wa Lacazette na Arsenal unamalizika mwaka 2022, baada ya kuwasili hapo kutoka kwa miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Lyon mwaka 2017.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 aliingia akitokea benchi na kufunga wakati Arsenal ikiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Wolves Jumamosi.

Lacazette ameanza katika mechi mbili tu za Arsenal katika mechi nane zilizopita na Arteta anatambua kwamba majaliwa ya raia huyo wa Ufaransa hayajamalizwa.

"Tunatakiwa kuzungumza na yeye kuhusu hisia zake na nini anachokifikiria. Kama nilivyosema, nina furaha juu yake," alisema Arteta.

"Yeye ni mchezaji ambaye mara zote nimekuwa nikivutiwa nae, hata wakati ambao sikuwa hapa, kwa sababu ya kile anachokileta kwenye timu; ubora wake, uwezo wake na kazi yake. Ngoja tuone.

"Kwa sasa tupo kwenye wakati muhimu. Ni wakati wa kuzungumza kuhusu hali ya mikataba. Bado tuna muda na tutafanya wakati muafaka ukifika."

Arsenal wapo nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya mechi 33 wakipitwa pointi tatu na Wolves waliopo nafasi ya sita.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO AFIKISHA MECHI 200 ZA USHINDI

## Asema ni bahati kwake kufanya kazi na klabu kubwa tatu duniani, lakini sio...

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesema sio makocha wengi wamekuwa na bahati ya kufanya kazi katika klabu tatu kubwa duniani, wakati kocha huyo wa Tottenham Hotspur akifikisha mechi 200 za ushindi kwenye Ligi Kuu ya England.

**Mourinho alisherehekea mafanikio hayo Jumatatu, wakati akiweka rekodi ya kushinda mechi 200 kwenye Ligi Kuu ya England kama kocha, baada ya Spurs kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Everton.**

Raia huyo wa Ureno alifikisha mechi 326 kwenye Ligi Kuu ya England, huku akimzidi gwiji wa Manchester United, Sir Alex Ferguson (322).

Mourinho alishinda mechi 140 za EPL katika vipindi viwili alivyokaa Chelsea - ambako alibeba mara tatu taji la Ligi Kuu na alishinda mechi 50 wakati akiwa pale United na Jumatatu alifikisha mechi 10 za ushindi pale Spurs tangu achukue mikoba ya Mauricio Pochettino.

"Sio makocha wengi wamefanya kazi na klabu kubwa nchini, na duniani," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Nilikuwa na bahati ya kutosha kufanya kazi na klabu kubwa tatu hapa nchini. Wakati unapokuwa kwenye klabu kubwa, ni rahisi kuwa na matokeo kama haya."

Tottenham walirudi kutoka kuchezea kichapo cha mabao 3-1 walichokipata kwa Sheffield United mara ya mwisho, huku bao la dakika ya 24 la Michael Keane la kujifunga ndio likawapa ushindi vijana hao wa Mourinho pale kwenye dimba la Tottenham Hotspur.

Spurs wapo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi, wakipitwa pointi nne kutoka nafasi ya nne na pointi moja na Arsenal waliopo nafasi ya saba ambao watakutana kwenye mchezo wa Jumapili.

"Nafikiri mchezo dhidi ya Arsenal mara zote utakuwa muhimu kwa sababu ni Arsenal," alisema Mourinho alipoulizwa kama Tottenham wataingia kwenye mchezo huo wakiwa na morali baada ya wachezaji wake, Hugo Lloris na Son Heung-min kuzozana na nusuru wazichape.

"Akili yangu ni muhimu kama tukishinda dhidi ya Bournemouth (Alhamisi). Kucheza na Arsenal, unakuwa na upinzani mkubwa na kwa sababu tunataka kushinda mechi yetu dhidi ya wapinzani wetu, jambo lile halikunifurahisha.

"Nataka mchezo dhidi ya Arsenal kuchezwa kama tunakwenda kushinda kitu fulani. Tunahitaji kushinda dhidi ya Bournemouth na baadaye dhidi ya Arsenal."

Golikipa wa Tottenham, Lloris na fowadi Son walibwatukiana wakati wakielekea mapumziko.

Hiyo ni baada ya tukio la Son kushindwa kumkaba Richarlison wa Everton ambaye alikaribia kufunga.

## ZISIKUPITE

### LAMPARD AWINDA KINDA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anamwania kiungo wa West Ham na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 21 katika kikosi chake hicho. ***(Times)***

### WAGOMBEWA EPL

MANCHESTER City na Manchester United zone zinawawania walinzi wa kati wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, na Milan Skriniar mwenye miaka 25, ambaye anaichezea Inter Milan na Slovakia. ***(Independent)***

### NYOTA AGONGANISHA ULAYA

CHELSEA na Real Madrid zote zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic zikijaribu kuzipiku Manchester United na Paris St-Germain kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 raia wa Serbia. ***(Gazzetta dello Sport, via Express)***

### OLE ATETA NA BEKI AKE

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer inaonekana alimwambia mlinzi wa kati wa Bournemouth, Nathan Ake kwamba, "tunahitaji beki wa kati anayetumia mguu wa kushoto," wakati wa mazungumzo yake na mlinzi huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 25 baada ya mchezo wao wa Jumamosi pale Old Trafford ambapo walishinda 5-2. ***(Telegraph)***

### PALANCE KUMSAJILI EDOUARD

KLABU ya Crystal Palace inatarajia kufanya uhamisho wa pauni milioni 25 kwa straika wa Celtic na Ufaransa, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 22. ***(Sun)***

### ALABA HAKIELEWEKI BAYERN

BAYERN Munich itamwachia David Alaba mwenye kuamua kama anataka kubaki au kwenda Ligi Kuu ya England. Mlinzi huyo wa kimataifa wa Austria mwenye umri wa miaka 28, mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2021e. ***(Mirror)***

### UPAMECANO KUBAKISHWA

RB Leipzig inatarajia mlinzi wake wa Ufaransa, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 21, ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal, atasaini mkataba mpya, wakati huu wa sasa utakapomalizika mwaka 2021. ***(Mirror)***

### JUVE YAJITOSA KWA JORGINHO

KLABU ya Juventus inaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa Chelsea na timu ya taifa ya Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 28, wakati dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto litakapofunguliwa. ***(Tuttosport, via Sun)***

### REAL MADRID KUTOSAJILI

Real Madrid inapanga kutofanya usajili mkubwa wakati huu wa majira ya joto kwa sababu ya athari ya mlipuko wa virusi vya corona. Badala yake klabu inatumaini kuongeza pauni milioni 190 kwa mishahara ya wachezaji, huku winga wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 30, akihusishwa kuondoka. ***(Marca, via Star)***

### SABABU HAKIMI KUONDOKA

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane ndio sababu ya kwanini mchezaji wa kimataifa wa Morocco, Achraf Hakimi mwenye umri wa miaka 21 kuondoka klabu hapo na kujiunga na Inter Milan, kwa mujibu wa wakala wake wa mlinzi huyo. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

## Yanga Princess yaipania Simba

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema amesema wanahitaji kufuta 'uteja' katika mechi yao dhidi ya Simba Queens kutokana na kufungwa kila wanapokutana kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Yanga inatarajiwa kushuka dimbani dhidi ya wenyeji wao Simba Queens mechi itakayopigwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena uliopo Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Lema alisema hawako tayari kupoteza mchezo huo na kuhakikisha wanapambana kupata matokeo mbele ya wapinzani wao hao.

Lema alisema kikosi chake kipo vizuri na wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya kutaka kulipa kisasi kutokana na kukubali kichapo wanapokutana na Simba.

"Hii ni mechi ya 'dabi', ni ngumu itakuwa ya ushindani mkubwa hatuko tayari kupoteza huu mchezo ni muhimu sana kwetu, tunahitaji kufuta uteja wa kufungwa kila tunapocheza nao," alisema Lema.

Alisema hawako tayari kupoteza mchezo huo na kuhakikisha wanajiandaa vizuri, ili kufuta mazoea ya kila msimu wanapoteza mechi dhidi ya vinara wa ligi hiyo, Simba Queens.

"Nawaheshimu wapinzani wetu, tunaendelea na mazoezi kwa kufanyia kazi upungufu wetu wa michezo iliyopita na hadi sasa hatuna mchezaji majeruhi wote wapo fiti," alisema Lema.

## Coastal haijashinda mapumziko corona

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Coastal Union ya Tanga, haijashinda mechi yoyote ile tangu Ligi Kuu Tanzania Bara iruhusiwe tena, baada ya mapumziko ya kupisha ugonjwa wa mlipuko wa Covid-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Tangu iliposhinda mabao 2-0 dhidi ya Lipuli, Machi 10 mwaka huu, Coastal imecheza mechi tano, ikitoka sare mbili na kufungwa mechi tatu.

Juzi Jumatatu, ikiwa kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, Coastal Union ilichapwa mabao 3-1 na kuendeleza rekodi yake mbovu, baada ya janga la corona.

Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Juma Mgonda amekiri ni kweli hawajafanya vizuri tangu waliporejea tena dimbani baada ya mapumziko ya corona, lakini akasema hali hiyo atairekebisha taratibu.

"Tukianngalia mechi dhidi ya Mbeya City, tumefungwa kutokana na makosa ya mabeki wangu, tena ya kujirudia, na kweli tukaadhibiwa," alisema Mgunda.

Hata hivyo, baadhi ya wadau wa soka nchini Tanga wanadai kuwa timu yao kwa sasa haichezi vema kutokana na kwamba wachezaji wao wameshajua kuwa hawashuki daraja, hivyo morali imepungua, lakini wapo wanaodai kuwa sababu kubwa ni baadhi ya wachezaji kutakiwa na klabu kubwa, wakiongozwa na Bakari Mwamnyeto na Issa Abushehe.



Vijana wakifanya mazoezi jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# SINGIDA UNITED YAAHIDI KUMALIZA LIGI KIVINGINE

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake tayari imeshateremka daraja, Kocha Mkuu wa Singida United, Ramadhani Nswanzurwimo, amesema kikosi chake kitaendelea kupambana kusaka ushindi katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zilizobaki.

**Kauli ya Nswanzurwimo imekuja siku chache baada ya kikosi chake kupokea kichapo cha bila huruma cha mabao 7-0 kutoka kwa Azam FC ya jijini, Dar es Salaam.**

Singida United bado iko jijini na leo itashuka dimbani kwenye Uwanja wa Azam Complex kuwakabili KMC.

Kocha huyo alisema wachezaji wake ambao ni vijana waliobakia kwenye kikosi hicho, wanaendelea kuimarika na mechi zinazofuata hazitakuwa nyepesi wa wapinzani wao.

Alisema akirekebisha makosa machache kwenye safu ya ulinzi, wataingia tofauti katika mechi zinazofuata za ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

"Wachezaji wangu bado hawana muunganiko mzuri, ni vijana na hawana pia uzoefu mkubwa wa kupambana kwenye ligi, ninaamini wanaendelea kujifunza na kuimarika," alisema kocha huyo.

Alieleza kama washambuliaji wa Azam wangekuwa makini zaidi katika mechi yao iliyopita, wangefunga idadi kubwa ya mabao tofauti na ushindi huo walioupata.

"Azam wamecheza kwa nidhamu kubwa pia wametumia uzoefu wao, kwa timu yangu haikuwa na uzoefu, kwa sababu kikosi ninachokitumia baada ya wengine kuondoka ni cha vijana, wengine wameshindwa kuvumilia kuishi bila mshahara," alisema Nswanzurwimo.

Singida United inaburuza mkia ikiwa na pointi 15 baada ya kushuka dimbani mara 33 wakati tayari bingwa wa msimu huu, Simba anakabidhiwa kombe kesho mkoani Lindi.

# *Mbabe, Mrate ulingoni Julai 25*

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Dullah Mbabe atapambana na Allen Mrate katika pambano la kuwania ubingwa wa Taifa wa ngumi linalotarajiwa kufanyika Julai 25, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Mbabe, Omary Perege, alisema bondia wake anaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kupata ushindi katika pambano hilo.

Perege alisema amemwandaa bondia wake kuonyesha kiwango bora ili kupata mkanda na vile vile kuwafurahisha mashabiki wanaomuunga mkono.

Alisema pambano hilo litawasaidia kuwajenga na kuwaandaa na mapambano mengine ya kimataifa baada ya kukaa bila kupigana kwa muda mrefu kwa sababu ya kujikinga na virusi vya corona.

"Pambano hilo litakuwa la raundi 10, limeandaliwa kwa lengo la kuwapima nguvu mabondia hawa, tukumbuke wamekaa muda mrefu bila ya kupata mechi, tunawarejesha kwenye ubora wao," alisema Perege.

Naye bondia Mbabe alisema anaamini ataendeleza rekodi nzuri ya kupata ushindi na hawana hofu yoyote dhidi ya mpinzani wake huyo.

"Nimejipanga vizuri kuwapa burudani mashabiki wangu, nawaomba waje kwa wingi siku ya pambano, sitawaangusha," alisema kwa kifupi bondia huyo.

Kambi ya Mbabe iko Mwananyamala jijini, ambapo anajifua pamoja na mabondia wengine chipikizi na wazoefu.

# Michezo

Jumatano Julai 8, 2020

Nipashe




Mourinho afikisha mechi 200 za ushindi

UKURASA 22




Golikipa wa Tottenham, Hugo Lloris akiokoa hatari langoni mwake wakati wa mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Everton kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur jijini London, uliopigwa Jumatatu. Spurs ilishinda 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Kagere straika tishio Ligi Kuu

**Na Somoe Ng'itu, LINDI**

LICHA ya kukaa muda mrefu bila ya kufunga mabao, benchi la ufundi la Simba, limesema hakuna straika mwingine wa Ligi Kuu Tanzania Bara anayefikia uwezo wa Mnyarwanda, Meddie Kagere, imeelezwa.

Kagere ndiye anaongoza kwa kupachika mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, akiwa amezifumania nyavu mara 19, akifuatiwa na Yusuph Mhilu wa Kagera Sugar ambaye amefunga magoli 12.

Hata hivyo straika huyo hajafunga bao hata moja tangu kurejea kwa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya mapumziko yaliyosababishwa na virusi vya ugonjwa wa corona kumalizika.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, aliliambia Nipashe Kagere ataendelea kuwa mmoja wa washambuliaji wenye ubora katika Ligi Kuu Tanzania Bara hata kama hatafunga mabao mengine katika mechi zilizobakia msimu huu.

Matola alisema mchezaji huyo amekuwa akitumia nafasi nyingi katika mechi na mchango wake umekuwa ni mkubwa kwenye kufikia malengo.

"Bado ni straika wa daraja la juu, akiwa uwanjani anakabwa na watu wawili au zaidi, wanajua uwezo wake, hata asipofunga anasaidia kuichezesha timu, naamini ni mmoja wa waliotufanyia kazi kubwa msimu huu," Matola alisema.

Kagere aliyetua Simba akitokea Gor Mahia ya Kenya, ndiye mfungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita, ambapo alifunga mabao 22.

# Simba yaahidi furaha Lindi

**Na Somoe Ng'itu,** LINDI

### ●●● Ni katika kunogesha sherehe za ubingwa, huku Yanga ikijiuliza tena kwa Kagera Sugar Kaitaba...

VIWANJA tisa vya hapa nchini vinatarajia kuwa na hekaheka za mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini macho yote yanatarajiwa kuelekezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa ambapo mabingwa wa msimu huu 2019/20, Simba watakapovaana na wenyeji wao, Namungo FC.

**Tayari Simba ilishatangazwa kuwa mabingwa kwa msimu wa tatu mfululizo na leo baada ya mechi hiyo watakabidhiwa kombe lao ambalo watalichukua moja kwa moja.**

Simba itashuka katika mchezo wa leo ikiwa na kumbukumbu ya kichapo cha bao 1-0 walichopokea kutoka kwa Kagera Sugar wakati wakikabidhiwa kombe la msimu uliopita, wakiwa mbele ya Rais, John Magufuli.

Namungo FC ambao wanashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza wataingia dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kufungwa magoli 3-2 na mabingwa hao walipokutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza jijini, Dar es Salaam, lakini kikosi hicho cha Kocha Mkuu, Hitimana Thiery, hakijapoteza mechi yoyote, kati ya michezo 17 iliyopita ya ligi hiyo pamoja na mashindano ya Kombe la FA.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, ameliambia gazeti hili kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na wamejipanga kupata ushindi ili kutoharibu sherehe za kukabidhiwa kikombe.

Sven alisema kila mchezaji yuko tayari na amewataka kuongeza umakini ili watimize malengo yao ya kufanya vizuri zaidi msimu huu.

"Tuko tayari kwa mechi, najua haitakuwa rahisi kutokana na wenyeji kuwa na timu nzuri pia, wanacheza kwa kasi na wanauzoefu pia na mechi kubwa, wana rekodi nzuri kama ambavyo sisi tunahitaji kuweka rekodi yetu, natumaini itakuwa mechi yenye kuvutia pia," alisema Mbelgiji huyo.

Nahodha wa timu hiyo, John Bocco alisema kila mechi kwao ni muhimu na wataingia uwanjani kusaka ushindi bila kujali wameshakamilisha hesabu za ubingwa.

"Tuko imara na tayari kwa mechi, hakuna mechi rahisi katika ligi, sisi ni mabingwa, lakini haimaanishi tutaingia uwanjani kukamilisha ratiba, tunataka ushindi wa kupokelea kikombe," Bocco alisema.

Luc Eymael, Kocha Mkuu wa Yanga, aliliambia gazeti hili safari na malengo yake ni kuona wanamaliza Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa katika nafasi ya pili na hilo litawezekana kama watashinda michezo yote mitano iliyobaki.

Kocha huyo alisema wanahitaji kupata heshima hiyo baada ya kushindwa kutwaa taji, huku wakijiandaa kuwaondoa watani zao kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA hapo Jumapili.

"Nimeongea na wachezaji wangu kuhusu mechi hii, nimewaambia tunatakiwa kuwafunga Kagera Sugar halafu ndio kuifikiria zaidi Simba, ingawa haitakuwa kazi rahisi, tumekutana mara nyingi na wamekuwa wakitusumbua, hata kesho (leo), hatutakuwa na kazi rahisi, tunatakiwa kupambana," Eymael alisema.

Kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa timu hiyo Mghana, Bernard Morrison atakuwapo katika mchezo huo baada ya kuikosa mechi iliyopita dhidi ya Biashara United ambayo ilimalizika kwa sare ya bila kufungana.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema anaijua vema Yanga na kama mchezo utachezwa kwa haki, pointi tatu zitabaki Bukoba.

"Nawajua walivyo, hawanisumbui kama tunacheza nao bila nguvu ya ziada, naahidi vijana wangu wataendelea kuonyesha soka la kuvutia na ushindani, subirini muda utaongea," Maxime alisema.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Azam dhidi ya Mwadui FC, Mbao vs Mtibwa Sugar, Ndanda vs JKT Tanzania, Alliance vs Lipuli, Mbeya City vs Polisi Tanzania, Biashara United vs Ruvu Shooting na KMC watawakaribisha Singida United.

Raundi ya 34 ya ligi hiyo itakamilika kesho kwa Tanzania Prisons kuwakaribisha Coastal Union kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042